ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita - Tarehe 30 Novemba, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hati mezani Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi Fedha za Umma na kuweka Masharti bora ya Kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo na kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali Nam. 12 ya Mwaka 2005.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na kuweka masharti bora ya Kudhibiti Usimamizi wa Fedha za Umma na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo na kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha Nam.12 ya mwaka 2005. Ahsante.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 80

Taratibu za Kuwashughulikia Viongozi Wastaafu

Mhe. Machano Othman Said - Aliuliza:-

Katika kutambua mchango mkubwa uliotolewa na Viongozi wa Kitaifa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayo Sheria ya Kuwaenzi Viongozi Wastaafu "*The Political Leaders Retirement Benefits Act. No. 2 of 2012*. Hata hivyo, pamoja na nia nzuri hiyo ya serikali, bado viongozi hao hasa wanaostaafu na cheo cha Makamu wa Rais au Spika wa Baraza la Wawakilishi, baadhi yao wanakuwa na utashi wa kisiasa wa kugombea nafasi ndani ya vyama vyao na nafasi ya urais wa Zanzibar.

(a) Kwa kuwa viongozi hao wanalindwa na Sheria hiyo ya Mafao ya Viongozi Wastaafu. Je, serikali haioni kwamba muda umefika kwa viongozi hao kubanwa kisheria wasigombee nafasi hizo.

(b) Kama serikali haina mpango huo haioni kwamba kuendelea kuwapa stahiki zote hizo wakati wanaendelea kufanya siasa na kugombea nafasi za juu za uongozi wa nchi ni kutumia ovyo haki ya wananchi.

(c) Kwa kuwa migogoro mingi ya kisiasa Zanzibar inasababishwa na viongozi wa aina hiyo, je, serikali haioni kwamba wakati umefika wa kuwa na Baraza la Ushauri litalowajumuisha viongozi hao badala ya kujiingiza wao wenyewe katika migogoro ya kutafuta uongozi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mheshimiwa naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Sheria ya Mafao ya Viongozi Wastaafu wa Kisiasa, Sheria Nambari 2 ya mwaka 2012 *"The Political Leaders Retirement Benefits Act, No. 2 of 2012",* kwa msingi wa kuwaenzi na kuwatunza viongozi hao baada ya kustaafu. Hali hii inatokana na kwamba, kwanza tunathamini mchango wao na kuutambua kwa kujitoa kwao katika kulitumikia taifa letu wakati wa kipindi chao cha uongozi. Sheria hii haikuzungumzia suala la kuwakataza viongozi hao kutokugombea nafasi nyengine zozote za uongozi ama katika serikali ama vyama vya kisiasa baada ya kustaafu kwao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba suala la kuchagua na kuchaguliwa ni haki ya Kikatiba na kwa kila mwananchi aliyefikia vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria. Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu cha 29(2) (a) na (d) kinaeleza sifa zinazohitajika kwa mgombea wa nafasi ya kiti cha Urais wa Zanzibar. Aidha, sifa na taratibu za kugombea nafasi za uongozi ndani ya vyama vya siasa huwekwa kwa mujibu wa Katiba za vyama husika.

Mhe. Mwenyekiti, aidha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina dhamira wala nia ya kumzuwia raia yeyote wa Zanzibar kugombea nafasi ya uongozi ile msingi kufuata sheria na kanuni zilizowekwa. Dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kukuza na kustawisha demokrasia nchini mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, majibu ni kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa wakati huu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni busara ya kuwabana Kisheria Viongozi wa Kisiasa Wastaafu wasitumie fursa yao ya Kikatiba ya kugombea Uongozi pale wanapoona inafaa.

(b) Haki ya kuwalipa Viongozi wa Kisiasa Wastaafu ni jambo la kisheria na halitokani na utashi. Hivyo serikali, itaendelea kuwalipa na kuwapa haki zao nyengine viongozi wao kama sheria ilivyoelekeza.

(c) Hakuna wazo la kuwa na Baraza la Ushauri la Viongozi Wastaafu kwa hivi sasa. Aidha, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hakwaziki kutafuta au kutaka ushauri kwa mtu yeyote na wala halazimiki kufuata ushauri huo kwa mtu yeyote.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Ni kweli kwamba katiba na sheria inawatambua viongozi hawa na kulipwa mafao yao. Lakini katiba na sheria pia inaundwa na binadamu na kwa kupitia Baraza hili. Kwa hivyo, katiba wakati wowote inaweza kubadilishwa na sheria inaweza kubadilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, haoni kwamba kuendelea na utaratibu huu kwa viongozi hawa kulipwa karibu asilimia 80 ya mapato ya viongozi waliokuweko madarakani, kupewa nyumba, usafiri na safari za nje, halafu ukifika wakati wa kugombea viongozi hawa wanagombea na kuitukana serikali hiyo hiyo ambayo inawapa fidia hizo kwamba ni tatizo. Kwa nini wasiamue moja kwamba ama wagombee au wakubali kupata mafao yao mpaka wamalize umri wa maisha yao. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, swali la msingi lilikuwa linauliza kwamba, serikali kama tunaona haja au hatuoni haja. Tumejibu kwamba serikali hatuoni haja ya kufanya mabadiliko ya kuwazuwia viongozi hawa kushiriki katika shughuli za kugombea nafasi za uongozi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tutambue serikali makini yoyote duniani kama ilivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haiwezi kuendeshwa kwa wimbi la hofu la mtu, ama wimbi la hofu la kikundi cha watu, serikali siku zote itafanya mabadiliko yawe ya maendeleo, iwe ya sera, ama sheria kwa msingi wa kuitazama jamii yetu tunayoiongoza na maslahi ya wananchi wetu kwa ujumla wake.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri, amesema kwamba viongozi wastaafu walikuwa wametoa michango mikubwa katika taifa hili, ni kweli tunakubaliana na hilo. Lakini hao hao baadhi ya wengine huilani serikali iliyoko madarakani na kutoa maneno yaliyokuwa siyo na pia bado wakaendelea kupewa yale maposho ambayo ni ya kustaafia.

Je, kuna hatua zinazochukuliwa kwa viongozi hawa ambao wametoa mchango lakini wakarudi wakailani serikali ile iliyopo madarakani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, viongozi hawa wanalipwa kutokana na utumishi wao waliokuwa wakiitumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wataendelea kulipwa kwa kutambua mchango wao walioutoa wakiwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunatambua nchi yetu imefungua ukurasa wa demokrasia patafika pahali tutashindanisha sera na mitazamo ya kisiasa, lakini imani yangu kwamba kiongozi yeyote mwenye kujielewa awe katika ofisi, ama awe amestaafu ni wajibu wake kuiheshimu, kuitii na kuisaidia serikali katika kuwatumikia wananchi wetu. Kama kuna kiongozi ambaye anakwenda kinyume na hivyo maana yake kiongozi huyo yeye mwenyewe atakuwa anajipunguzia sifa za kuitwa kiongozi.

Kwa hivyo, imani yangu kwamba kama kuna kiongozi yeye ni mwanadamu atachukua fursa ya kujisahihisha ili arudi katika mstari uliyonyooka kuona yeye ni kiongozi anapewa heshima na yeye ni wajibu wake sasa kuitunza heshima ile kulisaidia taifa letu katika harakati za maendeleo kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, haoni haja ya kutunga Kanuni ambayo itamuwajibisha kiongozi yeyote wa kitaifa ambaye amehalifu Sheria za nchi kutopata hizo *benefits* alizosema humu zinazostahiki.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, tumezungumzia suala la Sheria Nam. 2 ya mwaka 2012 yenye Madhumuni ya Malengo ya Kuwasaidia Viongozi wetu wastaafu katika nchi yetu kuweza kupata mafao ya kuweza kuwasaidia katika kuendeleza maisha yao. Msingi wetu mkubwa ni kutaka kuona, kuthamini na kutambua mchango wao wakiwa viongozi wetu katika kuleta maendeleo ya jamii yetu.

Sasa suala lililokuwepo kwamba hatuoni haja ya kufanya Kanuni. Naamini kwamba sheria iliyokuwepo inajitosheleza, inatoa muongozi vizuri na sio sheria hii inayoongoza nchi hii, Katiba ipo, sheria za viongozi zipo. Imani yangu kwamba sisi ni viongozi tutaendelea kutii sheria ziliopo ilituweza kutengeneza mustakbali mzuri zaidi kwa manufaa na maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na dharura aliyonayo Waziri wa Ardhi swali lake Nam. 51, nilikuwa naomba Wajumbe tumuachie Waziri wa Ardhi, apate atoe majibu kwa aliyeuliza halafu tutaendelea na taratibu.

Nam. 51

Mpango wa Serikali kwa Mji Mpya wa Tunguu

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-
Jimbo la Tunguu, ni katika majimbo ambayo yamepangiwa mkakati na serikali katika kuendeleza miji mipya na pamoja kuboresha makazi katika kufanya hivyo.

a) Ni kiasi gani cha fedha serikali imejipanga katika kuboresha Miundombinu ya maji, barabara na nishati katika makazi ya Jumbi, Tunguu na Bungi.

b) Kumekuwa na malalamiko ya wananchi ambao wao wamekuwa wakitumia maeneo hayo kwa ajili ya shughuli tofauti, ni utaratibu gani serikali inajipanga kwa wakazi wa hapo kuhakikisha na wao wanafaidika na hio rasilimali ya ardhi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake namba 51 kama ifuatavyo:

a) Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa eneo la Jumbi limepangwa kuendelezwa kupitia mradi wa *ADB* wa maji safi na usafi wa mazingira uliomalizika hivi karibuni chini ya ufadhili wa Benki ya Afrika na Serikali ya Mapinduzi kwa kujenga matangi na kuchimba visima katika eneo la Mkorogo na kulaza mabomba makubwa na madogo kutoka visimani hadi tangini na kutoka tangini hadi Tunguu ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Kazi inayoendelea hivi sasa ni serikali kusambaza mabomba madogo madogo katika eneo la Jumbi.

Kwa upande wa Bungi, Mamlaka ya Maji kwa kupitia mfadhili wa *Ras al Khaimah* tayari imeshachimba kisima na kazi zilizobaki ni kwa serikali pamoja na viongozi wa jimbo kuvuta umeme, ujenzi wa kibanda cha *pump*, ununuzi wa mabomba ambapo gharama zake zinakadiriwa kufikia 80,000,000/=.

Kwa upande wa Tunguu, Mamlaka ya maji kwa kupitia ufadhili wa *Ras al Khaimah* ilijenga tangi na visima katika eneo la mjengo na kazi zilizobaki ni kwa serikali pamoja na viongozi kuendeleza kwa uvutaji wa umeme, ujenzi wa kibanda cha kuendeshea *pump* na ununuzi wa mabomba.

b) Malalamiko ya wananchi kuhusiana na ardhi ni kwamba wizara imepokea taarifa hizo na inashughulikia na watapata stahiki kwa mujibu wa sheria. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ningependa nimuulize swali dogo sana Mhe. Waziri, kuhusiana na maeneo hayo niliyoyataja.

Mhe. Mwenyekiti, uhamiaji ambao unaendelea katika maeneo ya Tunguu, Jumbi pamoja na Bungi umekuwa ni mkubwa na pia serikali imegawa viwanja kwa ajili ya Wazanzibari na wananchi tafauti kutoka nchi yetu ili waweze kutumia rasilimali hiyo. Lakini pia hutokezea manung'uniko na malalamiko kwa wananchi hasa katika maeneo yao wao pia kwamba wanapokuja watu wahamiaji kutoka maeneo mengine kutoka nje wanagaiwa hivyo viwanja na wao wengine wanakosa hizo fursa.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni wananchi wangapi ambao wako katika maeneo hayo na katika jimbo langu watafaidika na hiyo rasilimali ya ardhi.

(b) Katika wananchi hasa katika eneo la Tunguu hadi hivi leo hawajawahi hata siku moja kuoga maji kwa kupitia katika bomba. Pamoja na hivyo visima vilivyochimbwa alivyovitaja na hasa katika eneo la Tunguu. Ni kweli na ni sahihi kwamba kisima kimeshachimbwa na *Ras al Khaimah*, lakini hakuna

mabomba, hakuna *pump* na kero kubwa kwa wananchi wangu wa jimbo langu ni suala la maji. Ni lini serikali hii ambayo imewaahidi wananchi hasa katika maeneo haya atanihakikishia kabla ya mkutano wa Bajeti unaokuja mwaka 2017 wa wananchi wa Tunguu wanapata haya maji. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jimbo la msingi ni kwamba, kazi iliyobakia kwa kushirikiana na viongozi wa jimbo eneo la Tunguu ni kupeleka umeme, ujenzi wa kibanda na kununua mabomba. Sasa tumekwenda katika jimbo lake kufanya ziara pamoja na yeye tukaona, kilichobakia ni kukamatana mikono kuona kwamba tunakamilisha vitu hivi kwa mahitaji haya ili wananchi wapate maji. Kwa hiyo, ukamilishwaji wa hitu hivi ndipo wananchi watapata maji.

Lakini kwa upande wa viwanja ni kwamba Sheria za ardhi zipo, aidha labda iwe sikumfahamu kama ni wepi ambao anawazungumzia ni wale ambao labda yatapita yale mabomba na wameathirika vile viwanja vyao, ama ni viwanja kwa ujumla. Lakini kwa hayo yote, sheria zipo na kwa mujibu wa sheria hataonewa mtu wala hapotendelewa mtu. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami napenda nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri. Pamoja na majibu yako mazuri uliyotueleza na kwa kuwa tatizo hili la maji lipo katika sehemu nyingi sana katika majimbo mengi, hususan Unguja na Pemba. Lakini na mantenki haya ambayo yaliyojengwa yapo mengi na ziara umefanya nyingi katika majimbo yote. Lakini kila unapopita unasema kwamba tutashirikiana baina ya viongozi wa majimbo pamoja na Serikali. Hebu tueleze ni lini hasa matatizo haya ya maji yatakwisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kama tumefanya ziara na tunaendelea kufanya kusudi kuangalia kila jimbo kuna kero gani na kutizama namna bora ya kuzitatua. Kwa hivyo, ni lini, maana yake baada ya kuona gharama halisi katika jimbo na kushirikiana na viongozi wa jimbo, tukakaa pamoja, tukazimaliza, maana yake hapo ndio itakuwa tatizo hilo halipo. Lakini kama tulivyokuwa tumesema, kwa vile maji ni uhai wa binaadamu na si binaadamu tu ila ni kiumbe chochote tutaendelea kusikia kwamba maji yanahitajika yanapigiwa kelele, lakini tusichoke katika kuungana mkono kusudi tuwatatulie watu wetu matatizo tuliyonayo. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri, amesema kwamba kupitia mfadhili wa *Ras al Khaimah* ambaye tayari kuna kisima ambacho kimechimbwa katika maeneo hayo yaliyotajwa. Lakini mbali na kisima hicho katika mradi wa *Ras al Khaimah* kumechimbwa visima vingi kwa Unguja na Pemba. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo unaosema, 'maji yatekwayo ndio yavaayo'. Yaani kile kisima kinachotumika ndio maji yanayowafaa wananchi. Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba vile visima vilivyochimbwa na *Ras al Khaimah* vinafanya kazi au zinatumiwa fedha kwa ajili ya kufanya kazi visima hivi ili kuwahudumia wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na Serikali inafahamu nia na dhamira yake na ndio maana kama atakumbuka vilikuwa 150 na sasa kama 10, 15 tayari vimeungwa katika jitihada hizo ambazo anazieleza. Lakini tukumbuke kwamba kwa ujumla wake haipungui bilioni saba ili kukamilika vile visima. Sasa Serikali inaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba namna inavyokuwa inaruhusu ndivyo vile visima vinaungwa.

Nam. 49

Kuwekwa "*Reserve Tank*" Eneo la Matuleni

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Eneo la Matuleni na Chanjamjawiri katika Jimbo la Chake Chake lina kisima cha *pump* ya maji lakini halina "*Reserve Tank*" mashine hiyo huwa inaharibika mara kwa mara na kupelekea wananchi kukosa maji ya uhakika.

Je, Serikali imejipangaje, kuhusu kuweka "*Reserve Tank*" ili kuondoa tatizo hilo kabisa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa Chake Chake swali lake nambari 49 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba vijiji vya Matuleni na Chanjamjawiri pamoja na vijiji jirani vinahudumiwa na kisima kimoja kilichopo Matuleni. Kwa bahati mbaya mradi huu haujakuwa na tangi la kuhifadhia maji na wananchi wanapata huduma ya maji moja kwa moja kutoka kisimani. Hata hivyo, zilianza harakati

za ujenzi wa tangi ambao ulisimama kwa sababu mbali mbali. Hivyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Maji imo katikia utaratibu wa kulifanyia mapitio ya usanifu wa mchoro na kujua mahitaji halisi ya ujazo wa tangi utakaoenda sambamba na mahitaji ya matumizi ya maji kwa wananchi wa Matuleini na Chanjamjawiri na hili linategemewa kujengwa katika eneo la Maalim Rabia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba, pale Chanjamjawiri maeneo yale hayajawahi kuwa na historia ya kuwa na tenki. Lakini ni eneo kubwa sana ambalo watu wanatumia maji ambayo tulikuwa tumewahamasisha wasianze kutumia visima ambavyo vinaweza kuwa havina uhalali au uhakika wa afya zao. Kwa hivyo, tukawaboreshea kwamba watumie maji ambayo yanatoka kwenye mabomba. Lakini maji ambayo hayana tenki ambayo *Reserve Tank* inaweza ikazuia *pump* inaweza ikajaza kwa siku moja, mbili, maji yale yakatumika *pump* ikapumzika. Sasa imebidi maji yale yanatumika kwa *pump* inapofanya kazi na *pump* inapokuwa haifanyi kazi maji yale hayapatikani na muda mwingi *pump* ile inachoka na kuharibika. Sasa mimi ningemuomba Mhe. Waziri, kama anakuwa hajawa tayari kutujengea tenki basi atuwekee mashine mbili; iwe tunapumzisha moja, wakati moja inafanya kazi au ikiharibika moja, nyengine moja inafanya kazi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tumesikia ushauri wake lakini kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba, baada ya mapitio na usanifu wa huu mchoro tutajua ni aina gani ya tenki na kwa muda itatuchukua, kwa hivyo, tutatizama kati ya muda huo na ushauri wake ambao aliousema.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri, napenda niulize swali la nyongeza. Visima vingi mashine zinaharibika na tunapotaka mafundi kutoka *ZAWA* mafundi wanakuwa ni kidogo wako wawili. Lakini utakuta Bumbwisudi mashine imeharibika, Matemwe mashine imeharibika na Makunduchi mashine imeharibika, lakini unapohitaji afike fundi anasema kwanza subiri nende huku na wananchi wengine wanapata tabu. Je, Wizara yako imejipangaje kutafuta mafundi wengine.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe.Mwenyekiti, tunao mafundi wengi ila wanaonekana kidogo kutokana na mahitaji na majimbo yetu yalivyo. Wizara imehakikisha kwamba kila Wilaya wanakuwepo kila aina ya watu wa *ZAWA*, nakusudia mafundi, operesheni,

cashier, aina yote ya watu ambao wanahitajika wanakuwepo kila Wilaya kusudi kupunguza haya matatizo na kuweza kuyakabili yanapotokea. Lakini niseme kwamba tumesikia ushauri wako wa kwamba bado wanahitajika wengine. *Inshaallah* tutazingatia. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Waziri, maji ni uhai katika maisha ya binaadamu na hata wanyama, lakini katika jimbo langu kuna kisima Shehia ya Mbuzini ambacho kisima kile kimezinduliwa kwenye mradi wa Mwenge hadi hii leo kisima kile hakijaanza kufanya kazi. Kisima kile kintarajiwa kutoa maji kupeleka pale Mbuzini na Ziwani. Je, ni lini kisima kila kitaanza kazi ili wananchi wangu wa Ziwani na Mbuzini waanze kupata maji na kuondokana na usumbufu wanaoupata.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hii taarifa tumeipokea na siku zote kama ninvyosema kwamba tutasaidiana, tutashirikiana na utayari wake kusudi kwamba tutapokwenda kwa ajili ya kukioni na kuona gharama gani zinahitajika tuungane mkono. Ahsante sana.

Nam. 16

Kunyimwa kwa Baadhi ya Wanafunzi kupata Haki ya Elimu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa kuwa kupata elimu ni haki ya Kikatiba kwa Mzanzibari.

(a) Je, ni kifungu gani cha sheria kinacho mzuia mtoto anayesoma katika skuli ya binafsi ambae kafaulu masomo ya Kidato cha Pili mtihani wa Taifa kuzuiliwa kujiunga na skuli za Serikali kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu.

(b) Je, Wizara haioni kwamba kufanya hivyo ni kumkosesha mtoto huyo haki yake ya Kikatiba ya kupata elimu.

(c) Je, ni hatua gani za Wizara zinachukuliwa kwa skuli ambazo zinawazuia wanafunzi wa Kidato cha Pili ambao wamefaulu mtihani wa Taifa wa SMZ na skuli hizo binafsi

wakawabakisha Kidato cha Tatu kwa visingizio kwamba wanafunzi hao hakufikia kiwango wanachokihitaji skuli hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Jimbo la Konde, swali lake namba 16 lenye sehemu (a), (b) na (c).

Kwanza napenda kutoa maelezo ya ufafanuzi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Elimu ya lazima ni haki ya msingi ya Wanafunzi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa inahakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata haki yao ya kupata elimu bora ya lazima. Pia, Serikali imeruhusu watu binafsi na mashirika yasio ya kiserikali kuanzisha skuli binafsi kwa madhumuni ya kuongeza upatikanaji wa nafasi za kujifunza.

Wanafunzi wote kabla ya kumaliza elimu ya lazima wanapaswa kufanya mitihani ya Kidato cha Pili na wanaofaulu huchaguliwa kuendelea na masomo ya Kidatu cha Tatu. Wanafunzi waliofaulu wanastahiki kuendelea na masomo ya Kidatu cha Tatu na Kidatu cha Nne katika skuli zao walizotokea iwe ya Serikali au ya binafsi. Hata hivyo, wapo baadhi ya wanafunzi waliomaliza Kidato cha Pili katika Skuli za Serikali na kushindwa ambao wamejiunga na skuli binafsi kwa kujiendeleza na hatimae kurudia tena kufanya mtihani wa Kidato cha Pili na kufaulu. Wizara inawapongeza wazazi na wanafunzi ambao baada ya kushindwa mitihani wanajiendeleza na baadae kufaulu. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

(a) Hakuna kifungu cha sheria kinachomzuia mwanafunzi anaesoma katika skuli za binafsi aliefaulu Mtihani wa pamoja wa Kidato kujiunga na skuli za Serikali. Kiutaratibu, mwanafunzi huyo anapaswa kuwasilisha maombi ya kujiunga na Skuli ya Serikali mara tu baada ya kutoka matokeo ya mtihani na kufaulu na atapangiwa skuli kulingana na nafasi zilizopo na sio kwa skuli atakayochagua yeye kama wengi wanavyofanya.

(b) Wizara haijamkosesha mwanafunzi yeyote haki yake ya kuendelea na masomo kama amefaulu Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili na amefuata taratibu zilizowekwa.

(c) Hakuna skuli ya Serikali iliyomzuia mwanafunzi aliefaulu Mtihani wa Kidato cha Pili asiendelee na masomo ya Kidato cha Tatu isipokuwa kwa wanafunzi waliojiunga tena katika skuli za Serikali baada ya kumaliza Kidato cha Pili, kwa njia za udanganyifu. Kuhusu Skuli binafsi zinazowazuia wanafunzi wao waliofaulu Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu, Wizara inapopata taarifa hizo huchukua hatua ya kuwaandikia wamiliki wa Skuli binafsi na kuwaagiza kuwaruhusu wanafunzi hao kuendelea na masomo yao. Napenda nitoe wito kwa wamiliki wa skuli binafsi kutowazuia au kuwafukuza wanafunzi waliofaulu Mitihani yao kwa kisingizio kuwa hawakufikia vigezo vilivyowekwa na skuli. Wataofanya hivyo watakuwa wanavunja sheria na Wizara itawachukulia hatua kali. Nawaomba wazazi ambao watoto wao wanapofukuzwa watoe taarifa Wizarani ili Wizara iweze kulifuatilia suala hilo na kuchukua hatua. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri, swali la nyongeza lenye vipengele (a) na (b). Kwanza, mimi ninashukuru sana Mhe. Waziri, kwenye jibu lake la msingi kukiri kwamba hakuna sheria inayomzuia mtoto kuendelea na masomo yake pale anapofanya mtihani na akafaulu. Lakini Mhe. Waziri na Baraza hili linataka litambue kwamba mimi mwenyewe hiyo kadhia ninayoizungumza imenikuta, si kwamba nimehadithiwa na mtu au kwa jambo jengine, mimi mwenyewe yamenikuta kwa mtoto wangu, lakini lililopita wacha lipishwe tuangalie mengine. Lakini kwa kuwa kwenye jibu lako umekiri kwamba kufanya hivyo ni kosa kisheria kwa skuli hizo kuwazuia watoto na skuli za Serikali kuwazuia kuendelea na masomo yao ya darasa la 11.

Je, ni mikakati gani ambayo Wizara itajipangia kuhakikisha kwamba jambo hili haliendelei na halitotokea tena kwa hizo skuli binafsi na skuli za Serikali. Kwa sababu Mhe. Waziri, ninakuhakikishia kwamba jambo hilo lipo na mimi mwenyewe ninayekwambia limenigusa. Je, ni mikakati gani itayohakikisha kwamba jambo hili halijirejei tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar, naomba urudi kwenye swali la nyongeza.

Mhe. Omar Seif Abeid: Swali la nyongeza ndio hilo Mhe. Mwenyekiti, naweka sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Uliza swali.

Mhe. Omar Seif Abeid: Hilo naliweka sawa, ndio ninaendelea na swali hivyo.

(b) Je, wanafunzi ambao na wazazi wameshindwa kuwaendeleza watoto wao kwenye skuli binafsi na ambao walikumbwa na kadhia hii, Serikali ina mpango gani wa kuwarejesha au itawapa nafasi za upendeleo wale wanafunzi ambao waliguswa na kadhia hii ili waweze kuendelea na masomo yao ya kidato cha tatu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, (a) ni kwamba Wizara imejipanga katika suala hili kuona kwamba halitokei ni kuwa wazazi wenyewe waelewe kwamba katika kujiunga na skuli kuna taratibu zake. Nina hakika Mheshimiwa aliyeuliza swali taratibu amezikosa, hakuna barua ambayo alimuandikia Katibu Mkuu Wizara ya Elimu kuomba nafasi hiyo. Kwa hivyo, tunawataka wazazi wakati wowote wanapotaka kujiunga katika skuli za binafsi, basi barua hiyo anaandikiwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, wala si Mwalimu Mkuu.Nadhani Mheshimiwa, amekwenda kwa Mwalimu Mkuu moja kwa moja, kwa hivyo, Mwalimu Mkuu aliyefanya hivyo yuko sahihi kumzuia kijana wako kwa sababu maombi lazima yaende kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu.

Inasisitizwa kwamba mara tu baada ya matokeo pale kutoka utaratibu uliopo kwamba, kijana wako amefaulu basi unamuandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu basi atakupatia nafasi katika Skuli ambayo itakuwa ina nafasi na wala si katika Skuli ambayo unataka wewe mzazi aende mtoto wako.

Swali jengine ni kwamba kwa sasa Wizara haina mpango ya kuwarejesha vijana hao kwa sababu kwamba wamekosea taratibu ambazo zingepaswa kufuata. Kwa hivyo, wasubiri mwakani waandike barua katika utaratibu unaohusika na nina hakika Wizara itawapokea vijana hao. Kwa hivyo, hapa nitoe wito tu kwa wazazi na walezi waelewe kuwa masuala ya kujiunga na mfumo wa skuli za kiserikali una taratibu zake na taratibu hizo ni pamoja na kumuandikia barua Katibu Mkuu. Ukifanya hivyo, hakuna skuli hata moja ya Serikali ambayo itamzuia mwanafunzi asisome. Ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu, kwa kujibu maswali kwa ufasaha sana, hongera sana. Pamoja na pongezi zangu hizo naomba niulize swali dogo la nyongeza. Wiki hii tunayoendelea nayo au mwishoni mwa wiki iliyopita Mhe. Waziri wa Elimu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Prof. Ndalichako ametoa agizo kwamba kuanzia sasa ili uwezo kujiunga na Chuo Kikuu lazima uwe umepitia *Form V* na *VI*, na sio utaratibu mwengine.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu ina tamko gani kuhusu kauli hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu haijapokea taarifa rasmi kutoka kwa Mhe. Waziri, anayehusika na masuala ya Jamhuri ya Muungano, wakati tutakapopata taarifa rasmi tutalijadili suala hilo na baadae serikali itatoa kauli yake.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, elimu ni msingi wa maisha ya binadamu, lakini kuna tatizo la kuzozana baina ya familia ya bwana Ayoub Suleiman wa Ndagoni na uongozi wa Skuli ya Ndagoni kutokana na kwamba wale waliokuwa wakitumia lile eneo la ardhi pale, na hivi sasa wanadai fidia ya ile miti yao kukatwa kwa ujenzi wa Skuli ya Ndagoni.

Je, ni lini familia ile watapatiwa fidia yao na kuna hatua gani zinazochukuliwa ili kuhakikisha kwamba mzozo huu unaondoshwa kabisa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, suala hili la umiliki wa ardhi katika Skuli ya Ndagoni mimi nalielewa vizuri kuliko anavyolielewa Mhe. Mwakilishi, na naelewa kwa sababu nimekuwa nikilifuatilia kwa karibu sana. Wizara inajaribu kulichunguza kwa undani zaidi suala hili kuona nani mmiliki halali, nani ana hatimiliki, nani ana *site plan* na nani ana nini. Nyaraka tulizonazo wizarani ambazo nimezifuatilia mimi mwenyewe hazitupi ruhusa ya kuwatambua watu uliowataja wewe kama ndio wamiliki wa shamba lile, waraka walioleta wizarani kudai shamba hilo umeandikwa kwamba unadai shamba la Shungi Pemba wakati eneo ambalo wanalidai sasa ni Ndagoni, pana tatizo hapo kwa kweli. Waraka walioleta wizarani kama wanadai kwamba shamba lile ni la kwao umeandikwa shamba la Shungi, Ndagoni na Shungi ni mbali mbali kwa kweli, na waraka huo ukitaka ukija wizarani tutakuonesha ili uridhike.

Kwa hivyo, kwa maana hiyo bado tunalifuatilia zaidi ili kupatia nani mmiliki halali na baadae tutalizungumza tena ili kuweza kulipa fidia wala sio kurudisha shamba, lakini kulipa fidia ya vipando vilivyomo mule.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo Mhe. Naibu Waziri, anieleze vizuri kwa sababu yeye mwenyewe aliniambia kwamba Ndagoni bado tu idhini ya Afisa Mdhamini wale wananchi ambao wana mzozo kutoa pesa zao, yeye mwenyewe aliniambia hivyo, leo ananiambia vyengine. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwakilishi, nadhani Mhe. Naibu Waziri, amesema yeye analijua kwa kina hilo suala na amesema yuko tayari kulishughulikia hilo suala. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi, nakuomba sana ukae umfate waziri ili hili suala litatuliwe.

Nam. 18

Tatizo la Kuzibwa Madirisha kwa Baadhi ya Skuli

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu suala hili limezungumzwa ndani ya chombo hiki kuhusu kuzibwa madirisha ya skuli na kusababisha wanafunzi wengi kuwa katika hatari ya kupoteza nuru ya macho kutokana na muangaza mdogo wanaoupata, kwa mfano Skuli ya Nyerere, Mwanakwerekwe “H”, Shaurimoyo na Kwamtipura.

(a) Je, ni sababu gani inayosababisha madirisha yasitiwe na kuwanyima muangaza wa kutosha watoto na kusababisha wanafunzi kuanguka kutokana na hali ya joto iliyomo katika madarasa hayo.

(b) Kama kuna mambo ya uhalifu yanayofanyika kupitia madirishani. Je, Serikali imeshindwa vipi kuweka ulinzi wa kukabiliana na matatizo hayo katika maeneo ya skuli ikiwemo walimu kurushiwa mayai viza.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye sehemu (a) na (b).

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi. Ni kweli kuwa baadhi ya skuli kama vile Skuli za Nyerere, Mwanakwerekwe “H”, Shaurimoyo, Kwamtipura na skuli nyengine, matundu ya madirisha yamezibwa kwa matofali na hivyo

kupunguza upitishaji wa hewa, kupunguwa kwa mwangaza na hatimae baadhi ya wanafunzi hupata athari ya macho na darasa kuwa na joto kali hasa nyakati za mchana. Hatua ya kuzibwa kwa matundu ya madirisha huchukuliwa na skuli kwa kushirikiana na Kamati za Skuli kutokana na kukithiri tabia ya baadhi ya watu kuwatupia wanafunzi uchafu na vinyesi wakati wa saa za masomo na baada ya saa za masomo. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

a) Baadhi ya matundu ya madirisha katika baadhi ya skuli kutokana na vijana wazururaji skuli kutupa uchafu wa aina mbali mbali kikiwemo kinyesi na mayai viza kupitia madirisha hayo wakati wa saa za masomo na baada ya saa za masomo kwa makusudi. Pia, baadhi ya wahalifu wamekuwa wakipita katika maeneo ya matundu hayo kuharibu au kuiba vifaa vya skuli yakiwemo madawati. Kuziba matundu ya madirisha ni njia moja wapo ya kukabiliana na kero hizo licha ya athari zinazotokea kutokana na kuzibwa kwa matundu hayo.

b) Wajibu wa kulinda na kutunza maeneo ya skuli na mali zake si wa Wizara ya Elimu au serikali peke yake, bali ni wajibu wa pamoja na wananchi. Katika baadhi ya maeneo, Kamati za Skuli wakishirikiana na uongozi wa Shehia na Kamati za Ulinzi Shirikishi zimefanikiwa sana kudhibiti vitendo vya uharibifu vinavyofanywa katika skuli zao. Napenda kutoa wito kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya skuili zinazofanyiwa hujuma hizo kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi ili kuwalinda wanafunzi wetu wasifanyiwe vitendo vya uharibifu kama kutupiwa uchafu na kuibiwa vifaa vya darasani na wahalifu.Vijana wanaofanya vitendo hivyo wengi wao wanajulikana na inawezekana sana kuwadhibiti na kuwachukulia hatua pindipo wananchi wataondoa muhali. Ahsante.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuuliza swali la nyongeza. Je, Mhe. Naibu Waziri, kuziba kwa madirisha hayo hamuoni kwamba mutawasababishia matatizo wanafunzi kwa kuwapunguzia nuru ya macho na baadae kupelekea kupata ulemavu wa uoni hafifu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, tunaona kwamba athari ipo ingawa sio kubwa kiasi hicho kwa sababu uzibaji ule wakati mwengine unafanyika katika matundu ya upande wa nje, upande wa ndani ya skuli una fursa ya kupata hewa safi na mwangaza. Lakini tumejaribu kuangalia katika baadhi ya maskuli ambayo tumeziba labda tumeacha nafasi

ndogo ili kupitisha mwangaza, basi nafasi hiyo hiyo inatumiwa na wahalifu kupenya na kutuharibia mali za skuli. Kwa hivyo, nafikiri suluhisho kubwa ni kwamba wananchi kushirikiana pamoja kuzuia uhalifu huu ili baadae skuli ziweze kupata mwangaza na hewa safi, nafikiri hili ni suluhisho peke yake. Lakini hata hivyo, tutajaribu kufanya utafiti wa kina zaidi, kwa sababu sasa hivi ni *assumption,* yaani tunadhani tutafanya utafiti wa kina zaidi ili tuone kiasi gani athari ipo.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri katika eneo hili la kudhibiti hivi vitendo ambavyo sio vizuri kwa wanafunzi wetu. Lakini Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu hayo, ukizingatia skuli zetu nyingi mazingira yake hayako vizuri hasa kutokana na kukosekana kwa uzio. Kwa mfano, ukienda hata Chuo cha Amali Mkokotoni, Vitongoji kule Pemba na skuli mpya zilizojengwa juzi hazikuzingatia pia uwepo wa uzio ambao ni sehemu moja ya kuwepo kwa ulinzi katika skuli hizo au Vyuo hivyo.

a) Je, ni lini serikali itazijengea skuli hizi uzio ili kuanza na hatua ya ulinzi uliobora kwa kuepuka haya waliyoyasema wenzangu.

b) Kwa kuwa serikali ina azma kupitia Ilani ya CCM kujenga skuli karibu 11 katika Ilani ya CCM, wizara yako imelizingatia suala hili la kuziwekea uzio skuli hizi ili kuja kuepuka uharibifu wa skuli hizi ambapo zitakapojengwa kama vile inavyotokezea katika skuli mpya zilizojengwa hivi karibuni.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, tunakubali kwamba skuli nyingi hazina uzio jambo ambalo pia limekuwa kivutio zaidi kwa wahalifu na waharibifu wa mali za skuli. Lakini niseme kwamba lini serikali itajenga uzio, ni kwamba huo ni mradi mkubwa sana na kwa sasa tunajaribu kuzihamasisha skuli binafsi kupitia wahisani mbali mbali kujenga uzio, na baadhi ya skuli zimeshaanza kufanya kazi hiyo na tunapongeza sana skuli ambazo zimefanikiwa kuanza kujenga uzio. Lakini katika kiwango cha serikali kuu ni kwamba bado suala hili linahitaji bajeti maalum na *In shaa Allah* itakapopatikana tutalifanyia kazi.

Kuhusu skuli mpya zitakazojengwa, hizi ni skuli ambazo ni za miradi, kwa hivyo, tunafikiria kwamba katika skuli mpya ambazo tutajenga suala la uzio litafikiriwa. Ninaposema zitakazojengwa ni kwamba hizo ambazo hatujafunga

mikataba nazo, lakini hizi ambazo tayari tumeshafunga mikataba zitaendelea kujengwa bila ya uzio. Lakini kuanzia sasa zitakazofungwa mikataba na katika bajeti zetu tutaingiza sehemu ya uzio. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kuna taarifa na matangazo, kwanza kabisa Waheshimiwa Wajumbe, tunapewa taarifa kwamba kuna Mhe. Said Omar Said wa Jimbo la Wingwi amefiliwa na mtoto wake, maziko yatakuwa leo saa saba mchana Viwanja vya Magereza Tomondo na kuzikwa Mwanakwerekwe.

Tangazo jengine kuna taarifa ya hitma, tunajuilishwa kwamba ile hitma ya wafanyakazi wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi waliokwisha kutangulia mbele ya haki hivi karibuni iliyokuwa isomwe baada ya Adhuhuri hii leo, sasa itasomwa leo baada ya Alaasiri. Hitma hiyo itasomwa hapa hapa katika Msikiti wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Chukwani.

Taarifa nyengine inahusu wageni, wageni tulionao ni wageni kwa ajili ya mafunzo wanatoka Chuo cha Utawala wa Umma (*IPA*) jumla yao ni saba, wapo hapa Barazani kwa mafunzo ya vitendo (*Field Attachment*) katika fani ya *Record Management,* naomba wasimame. Karibuni sana.(*Makofi*)

Nam. 36

Uendelezwaji wa Mashamba ya Mpira – Zanzibar

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza:-

Kwakuwa mashamba ya mipira yaliyopo Zanzibar ni moja kati ya mashamba ya serikali ambayo yanaingiza mapato katika nchi yetu ambapo wastani wa hekta 1,270 zililimwa (Unguja 637 na Pemba 633) na wastani wa tani 5,500 za utomvu zilizalishwa kwa kila mwaka kwa miaka mingi kuanzia mwaka 1985. Na kwakuwa sasa hivi imeonekana mashamba haya yamekodishwa kwa watu binafsi na kuonekana kuwa hayana matunzo ya uhakika, hayafanyiwi usafi, yamevamiwa, miti mingi imekufa na pia uvunaji mbaya.

(a) Je, serikali haioni kuwa sasa ni wakati wa kuwa na udhibiti mzuri wa mashamba haya pamoja na upandaji wa miti mipya.

(b) Je, tokea kuanzishwa mashamba haya ni miti mingapi imekufa na miti mingapi mipya imeshapandwa.

(c) Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea serikali kushindwa kulimiliki wenyewe shamba hili na kuliendeleza badala ya kulikodisha kwa wawekezaji.

Mhe. Waziri ya Fedha na Mipango – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha mashamba ya mipira mwaka 1975 kama sehemu za jitihada zake za kupanua zaidi shughuli za kilimo cha biashara ili kuwa na mazao mengine ya biashara zaidi ya karafuu na nazi. Kwa ujumla, mashamba haya yana ukubwa wa hekta 1,200. Mashamba haya yamepitia usimamizi tofauti ukiwemo wa serikali na kampuni binafsi. Mara ya mwisho mashamba yalikodishwa kwa Kampuni ya *Agrotex* ya hapa Zanzibar, iliyoajiri karibu watu 800. Mashamba yana miti ya mipira ambayo imeshafikia upeo wa uzalishaji wake kutokana na umri wake mkubwa na kuvunwa sana ambapo uzalishaji wa utomvu wa mpira umepungua kutoka wastani wa tani 5,500 hadi tani 800 kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nijibu maswali ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Tayari serikali imeamua kusitisha Mkataba na Kampuni ya *Agrotex* na kuyarudisha mashamba serikalini. Serikali pia inatafakari matumizi bora zaidi ya mashamba hayo kwa dhamira ile ile ya kutumika kwa ajili ya mazao mbadala ya biashara ili kusaidiana na zao la karafuu. Mwaka 2013, serikali imefanya uhakiki (*verification*) wa mipaka ya mshamba hayo na kuyaingia katika daftari la kudumu la mali za serikali.

b) Hakuna miti iliyopandwa tokea kukamilisha kwa mashamba hayo. Aidha, hakuna sensa iliyofanyika kujua idadi ya miti iliyokufa na kubaki hadi sasa.

c) Bado mashamba haya yanamilikiwa na serikali. Sababu zilizopelekea kuyakodisha kwa kampuni binafsi ni uamuzi wa serikali wa kujiondoa katika shughuli za moja kwa moja za biashara na kujikita katika kazi za msingi za serikali na utoaji wa huduma kwa jamii.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake, lakini nina swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa mashamba haya yeye anasema kwamba yamesharudi serikalini na hayapandwi miti ya kudumu. Je, yuko tayari mguu kwa mguu twende mimi nikamuoneshe miche ya mikarafuu ambayo kuwa imo ndani ya shamba tayari ambalo lina vikuta.

b) Atakubaliana na mimi Mhe. Waziri, kwamba mashamba haya kwa vile yamekuwa kama ni shamba la bibi kila mmoja anapita anafanya anavyotaka. Sasa kuyabadili tupande mazao mengine kama vile *vanilla*, hiliki na mazao mengine yanayofanana na hayo, ambayo yanafika katika shamba hilo au kuendeleza miche ya mikarafuu, anakubaliana nami suala hilo.

Mhe.Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema mashamba haya tayari yamesharudishwa serikalini na hivi sasa tuko katika mazungumzo na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ule mkataba unafutwa rasmi kisheria. Kwa hiyo, hilo la mwanzo.

La pili, inawezekana kwamba wapo watu ambao wamepata mazao mengine na hata juzi nimeona katika lile shamba la Tumbe, kuna baadhi ya wananchi wanapanda mazao mengine ya biashara kwa mfano *vanilla*. Kwa hivyo, inawezekana kwamba kuna mashamba ambayo yamepandwa miche ya mikarafuu. Lakini kama nilivyosema kwenye jibu la swali mama ni kwamba, serikali inatafakari namna bora ya kuyatumia mashamba hayo. Sasa tusubiri hadi hapo serikali itakapofanya uamuzi wa kwamba mashamba haya yatatumikaje, basi mabadiliko ya matumizi yatafanyika kufuatana na muongozo utakaotolewa na serikali.

Pamoja na hilo niko tayari kufuatana na Mhe. Shehe Hamad Mattar, kuyatembelea mashamba hayo, kwa sababu huo ni wajibu wetu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Waziri, kwa kuangalia tunakotoka, tulipo na tunakokwenda. Sasa tukiangalia kwamba kuanzia mwaka 1975 mashamba haya yalianzishwa kwa kuwa serikali inategemea ipate faida kwa kuendesha mambo yake ya huduma kwa jamii, lakini kwa bahati mbaya siku zinavyokwenda mapato yanapungua na mimea pia inafifia.

Je, kwa kuzingatia kwamba mkataba umefutwa na mwekezaji huyo aliyekuwa anaendesha mambo haya ya mashamba ya mipira. Kwa hivi sasa nani

mdhamini ambaye analinda angalau kuangalia usalama wa maeneo ya mashamba yetu kwamba wahalifu wasitokee kuyafanyia hujuma.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, tunataka kujua nani hivi sasa anayatunza mashamba hayo kwa Kiswahili chepesi. Ni kwamba mashamba hayo yako serikalini kama nilivyosema na mashamba hayo yako kwenye uangalizi wa Wizara ya Fedha na Mipango. Lakini kama hivi tulivyopata taarifa hivi karibuni hasa kwa lile shamba la Tumbe, wale waliokuwa wakifanya kazi pale hivi sasa bado wanaendelea kulitunza shamba lile, lakini vile vile wanaendelea kuvuna mali inayotokana na shamba lile.

Jibu langu ni kwamba, pamoja na mazingira hayo yote, serikali inayatambua na inayazingatia katika kutafuta mustakabali mzuri wa matumizi ya mashamba hayo.

Nam. 155

Wawekezaji Kutotekeleza Ahadi zao

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anastahili pongezi kwa hatua yake aliyochukuwa ya kutatua mzozo wa wananchi wa Matemwe Mbuyu Tende na Kijini, Mkoa wa Kaskazini Unguja, ambao wanadai fidia ya ardhi yao kutoka kwa mwekezaji wa "*Penny Resort*". Hata hivyo, kwa kuwa suala hilo limechukuwa muda wa miaka mitano wananchi hao wanadai fidia hiyo waliyoahidiwa na mwekezaji huyo pamoja na mambo mbali mbali na kuzusha malalamiko hayo.

(a) Je, serikali inachukuwa hatua gani kwa wawekezaji ambao wanatoa ahadi na kushindwa kuzitekeleza kwa muda mrefu.

(b) Mbali na kadhia hiyo ya mwekezaji wa Matemwe, serikali inatambua migogoro baina ya wawekezaji na wananchi katika maeneo mengine.

Mhe. Waziri ya Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 155 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba viongozi wetu wakuu wa nchi akiwemo Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, wanastahili pongezi kwa jitihada zao za kutatua matatizo ya wananchi wa Unguja na Pemba. Naomba nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu hawa kwa jitihada zao wanazozichukua.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali lake, naomba uniruhusu kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa *"Amber Resort"* unaotekelezwa na Kampuni ya "*Penny Royal*" (*Gibraltar Limited)*" una dhana ya kuendelea utalii wa hadhi ya juu na mji wa kifahari katika eneo la Muyuni huko Matemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Katika uwasilishaji wa dhana hiyo wakati wa kuomba kuidhinishwa kwake mradi huu kwa Mamlaka ya Uwekezaji, mradi huo uliruhusiwa kutekeleza ujenzi wa hoteli tatu za nyota tano *(5 Star Hotels)* pamoja na uwanja wa gofu katika eneo lenye ukubwa wa hekta 162.34. Hata hivyo, katika nyakati tofauti kampuni hiyo kwa kuongozwa na baadhi ya watu, imekuwa ikilipa moja kwa moja fidia kwa wananchi wa maeneo ya Matemwe kwa nia ya kuongeza ardhi na kubadilisha dhana ya mradi huo. Hadi sasa eneo hilo limefikia hekta 411.92. Serikali husaidia kutatua changamoto kwa wawekezaji na wananchi kila zinapojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Pale inapotokea haja ya kuwekeana adadi kwa maandishi baina ya mwekezaji na wananchi au serikali, serikali hutoa maelekezo ya namna ya kuratibu utekelezaji wa ahadi hizo na huchukua hatua kulingana na makubaliano ya ahadi hizo. Sheria inaruhusu kufuta kwa Hati ya Uwekezaji iwapo Mwekezaji amekiuka masharti ya kisheria ya uwekezaji.

b) Serikali inatambua kuwepo kwa migogoro kadhaa kati ya wawekezaji na wananchi kwa sababu mbali mbali, na huchukua jitihada zinazopaswa kuchukuliwa za usuluhishi kadri inavyojitokeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Rais wetu, tumpongeze Makamu wa Pili wa Rais na tuipongeze serikali kwa jumla kwa kuhakikisha kwamba katika njia kuu ambayo tunapatia riziki yetu na wananchi wetu ni utalii. Lakini nawashukuru viongozi hao kwa juhudi zao za kuhakikisha kwamba linapotokea tatizo linasuluhishwa ili kuleta maendeleo katika jamii yetu.

Je, kwa kuwa kuna mambo madogo madogo Mhe. Waziri, kasema baadhi ya maeneo, hili limekwisha, kuna mpango gani wa makusudi jamii ya maeneo yale kushirikishwa kuzungumza ili kutoa nafasi kwa wawekezaji ili kukuza pato letu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza migogoro tujue chanzo chake kikubwa kinatokea pale wananchi, ama mwekezaji anapokuwa hana uelewa wa kutosha wa sheria na taratibu ziliopo. Lakini vile vile hata kwa wananchi pia kwa kutelewa taratibu na sheria zilizopo nao hujiingiza kwenye matatizo ya migogoro ya ardhi. Kuna wakati ambapo kwa makusudi watu wanaelewa sheria lakini wanakiuka kufuata sheria hizo, sasa migogoro inatokea katika hali hiyo. Serikali itaendelea na juhudi ya kuelimisha, kwanza kuwaelimisha wawekezaji lakini vile vile kuwaelimisha wananchi juu ya sheria na taratibu zilizopo zinazowaongoza wawekezaji ili kuepukana na migogoro baina ya wananchi na wawekezaji hao.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Lakini kabla sijauliza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa majibu yake fasaha juu ya masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo la uelewa juu ya taratibu, sheria na mambo yanayohusiana na uwekezaji. Hata sisi Wajumbe wa Baraza tuna upungufu katika kuelewa masuala hayo. Labda nimuulize Mhe. Waziri, suala hili analifahamu kwamba tuna upungufu huo wa uelewa na lini anaweza kutoa semina kwa Wajumbe wa Baraza hili ili kuweza kuwa na uelewa mpana utakaotufanya tusiingie katika mambo ambayo hatuyajui. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naamini Mhe. Mwakilishi atakuwa na uhakika kwamba serikali inachukua jitihada kubwa sana za kujenga uelewa wa Wajumbe wa Baraza hili. Semina mbali mbali zinafanyika na hata masuala ya uwekezaji yameshafanyiwa semina kwenye Mabaraza yaliyopita na hata hili, lakini nimuhakikishie pale itakapotokea haja ya kufanya semina basi serikali kupitia wizara na taasisi zake tuko tayari kuwafanyia Waheshimiwa Wawakilishi, semina hiyo katika yale maeneo ambayo tunahisi bado uelewa unahitajika kwa Waheshimiwa Wajumbe. Kama

nilivyosema kwamba bado tutaendelea kutoa taaluma kwa wananchi lakini vile vile na wawekezaji.

Nam. 41

Kuimarishwa kwa Kilimo Nchini

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali imepania kukuza sekta ya kilimo nchini ili kuleta mageuzi ya kuichumi na kijamii hadi kufikia uchumi wa kipato cha kati mwaka 2020, kwa kuweka mikakati mikubwa katika nyanja mbali mbali za kiuchumi ikiwemo kilimo. Na kwa kuwa sasa hivi Tanzania Bara wameweza kulima kwa kujitosheleza wenyewe jambo ambalo serikali imezuwia kuagiza mchele kutoka nje kwa sababu kinachovunwa kinajitosheleza.

(a) Kwa ugawaji huu wa kila Shehia kupatiwa vipolo saba vya mbolea, dawa za kuulia magugu na mbegu. Je, serikali inadhani kuwa itafikia malengo kama waliyofikia wenzetu Tanzania Bara.

(b) Je, serikali imeweka mikakati gani endelevu katika kuimarisha kilimo nchini kivitendo.

(c) Je, ni matrekta mangapi mazima yanayofanya kazi ambayo yanatumika kwa kilimo sasa hivi na ni lini serikali itaongeza matrekta kwa ajili ya kuimarisha kilimo nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, wizara inapitia upya mfumo wa utoaji ruzuku wa pembejeo ili kuwezesha wakulima kupata idadi halisi ya pembejeo zinazotosha kwa eneo na kuondokana na tatizo la kupatiwa idadi ndogo ya pembejeo hizo. Aidha, wizara inaendelea na mpango wa kutoa taaluma kupitia kwa mabwana na mabibi shamba katika Shehia pamoja na miradi kama *ASSP/ASD-L*, na *ERPP* kwa wakulima wa mazao mbali mbali yakiwemo ya chakula na ya kibiashara, ili kuongeza uzalishaji wa chakula. Aidha, wizara ina mpango wa kuongeza miundombinu ya maendeleo ya umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, hadi sasa tunayo matrekta yanayofanya kazi 20 kwa mgao kama ifuatavyo:14 Unguja na 6 Pemba. Aidha, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ina mpango wa kununua matrekta 20 kutoka katika Kampuni ya *MAHIDRA MAHADRA* ya INDIA, taratibu za uwekaji sanini umeshakamilika na muda mfupi kutoka sasa matrekta hayo yanatarajiwa kuingia nchini.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, naomba naomba niulize swali la nyongeza lenye (a) na (b). Kwa kuwa kilimo cha kutegemea mvua ambacho tunakitegemea sana wakulima kinaanza kupitwa na wakati, na kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji maji ndio ambacho kinaweza kutukomboa ili kuweza kujitosheleza kwa chakula.

(a) Je, Mhe. Waziri, atakubaliana nami kwamba kulibadili bonde la Msaani, Pemba ambalo kuwa limo katika Jimbo la Mgogoni lenye ukubwa wa ekari 310 kulifanya la umwagiliaji maji ili tuweze kujitosheleza kwa chakula na mboga mboga.

(b) Je, Mhe. Waziri, anafahamu kwamba katika jimbo langu kuna bonde la Kwa Tovu Kiongoni, Pemba tayari limeanza kuvamiwa na maji chumvi kiasi ambacho wakulima wanaharibikiwa na mazao yao mbali mbali. Kama anafahamu, je, ni hatua gani alizochukua kwa kushirikiana na Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, swali lake la mwanzo kama alivyosema hili tunatarajia kama tulivyosema tunataka kuongeza maeneo ya umwagiliai maji. Kwa hivyo, itategemea ule mpango wa fedha. Hivyo, linaweza kuwemo bonde hilo na kulifanya la umwagiliaji maji au pengine lisiwemo. Lakini tunatarajia kwa mujibu wa fedha na mradi wetu wa *Exim Bank* utakapokamilika basi kama limo ndani ya *list* basi litakuwa kwenye umwagiliaji maji.

Swali lake la (b), amesema bonde lake linaingia maji ya chumvi. Hili nitaomba twende mimi na yeye kufanya ziara ili anioneshe na maafisa wetu tutaweza kuwashauri na kusikiliza ushauri wake.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru na namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu ya ufasaha kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuhusu bonde la Msaani kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba liliingia katika mpango wa *Exim Bank*, na kwa kuwa mpago huo sasa hivi kidogo umechelewa tuna mpango wa kuwashirikisha sekta binafsi pamoja na wakulima wenyewe namna ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji maji. Hivi sasa tuko kwenye mazungumzo na hatimaye tutawasilisha rasmi serikalini mpango mzima wa kuweza kuingiza watu binafsi kuweza kuimarisha mpunga katika mabonde mbali mbali kwa njia ya kumwagilia maji.

Vile vile, hata jana tulikuwa pamoja na Tume ya Mipango kuona kwamba tunaweza kutumia utaratibu wa *drip irrigation* ambao unaweza kusaidia sana katika suala zima la umwagiliaji maji kwa kutunza maji vizuri. Lakini pia tuna mpango wa kutumia uvunaji wa maji ya mvua ambayo na yenyewe yatasaidia sana katika kuondosha tatizo la ukame ambalo linatukuta kila wakati mashamba yetu.

Kuhusu shamba ambalo limevamiwa na maji chumvi kwa bahati nzuri mimi mwenyewe nimefika, nimekagua, kuna mambo mawili ambayo tungependa hata wananchi watusaidie. Kwanza serikali kwa kupitia *TASAF* walisaidia fedha kwa ajili ya kujenga uzio utakaosaidia kupunguza maji ya chumvi kuingia. Lakini vile vile na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa si chini ya shilingi 70 milioni kuendeleza katika kazi hiyo. Tatizo liliyopo lile tuta ambalo limejengwa wananchi wamegeuza barabara wanapita na matokeo yake maji tena yanaendelea kuingia. Tunauomba uongozi tusaidiane katika hili na hivi sasa tumepata utaalamu mwengine kutoka Marekani ambao utatusaidia katika maeneo yote ambayo yameingia maji ya chumvi namna gani tunaweza kukabiliana na tatizo hilo.

Kwa hivyo, serikali inachukua hatua lakini tunaomba sana ushirikiano wa wananchi, pale ambapo serikali imechukua hatua kuweka miundombinu ya kuzuiya maji hayo basi yasiibomoe ili maji yasiweze kuingia katika maeneo hayo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Nam. 116

Uimarishaji wa Chuo cha Kizimbani

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:-

Chuo cha Kilimo Kizimbani ni Chuo kinachotegemewa na jamii nzima, kwa kuzingatia msemo usemao “Kilimo ni uti wa mgongo”. Pia, katika chuo hicho tunatambua kwamba ndio chanzo cha wataalamu.

Je, serikali imejipanga vipi katika kurejesha uhalisia wa Chuo cha Kizimbani kwa kuimarisha uzalishaji mazao kama machungwa, chenza jem, ndimu tamu, mabalungi, na kadhalika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake namba 116 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli 'Kilimo ni uti wa mgongo' na Chuo cha Kilimo Kizimbani ni chanzo cha wataalamu wa fani za kilimo na mifugo hapa nchini. Ni tegemeo la Wazanzibar wengi ambao wamejiajiri katika Sekta ya Kilimo takriban asilimia 70.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia wizara yangu imejipanga katika kurejesha uhalisia wa Chuo cha Kizimbani kwa kukamilisha Mpango Mkakati wa miaka kumi (2017-2026) ambao utawekeza katika miundombinu, rasilimali watu na teknolojia za kisasa ambazo zinakwenda sambamba na mazingira yetu.Teknolojia hizi zitatoa fursa ya kuimarisha uzalishaji wa mazao ya jamii ya machungwa na mengineyo.

Aidha, chuo kinawashirikisha wanafunzi katika masomo yao ya vitendo ili kuwajengea uwezo wa masomo yao na kurejesha mandhari ya Kizimbani. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kutokana na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini pia naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

(a) Mhe. Spika, maelezo nimeyafahamu vizuri lakini napenda unifahamishe labda Mheshimiwa, Chuo cha Kizimbani kina eka ngapi

ambazo zimetengwa kwa makusudi kwa kuotesha vile vipando vipya au ile miti mipya ya matunda.

(b) Mhe. Waziri tunafahamu kwamba Chuo cha Kizimbani mwanzo kilikuwa kina wafanyakazi ambao walikuwa wanaotesha miti hiyo ya matunda na mazao mbali mbali ambapo kipindi hicho hata hiyo Tenkolojia ilikuwa haijafika na miti hiyo ilikuwa inakuwa na wananchi walikuwa wanafaidika na mazao hao ya matunda.

Lakini sasa hivi miti hiyo kiufupi haiko, kama tunafahamu kulikuwa na matunda kama chenza jemu, pili pili doria, chenza kali, kuna mazao mengi tu kiufupi. Lakini miti hiyo sasa hivi haipo kabisa.

Je, unatwambia nini wananchi wa Kizimbani au wananchi wa Zanzibar kwa ujumla sote ili kuweza kuirejesha miti ile na kuweza kuweza kukirejesha Chuo cha Kizimbani kwenye uhalisia wake. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Ushirika:

(a) Mhe. Mwenyekiti, suala lake la mwazo kuhusu eka hili naomba nitakujibu kwa maandishi kwa sababu tayari tumeshapima eneo la Kizimbani tunalo na ramani yake. Kwa hiyo, kutokana na kwamba suala lako la takwimu basi nitakujibu wa maandishi.

(b) Hii miche uliyoitaja kabla sijamjibu Mheshimiwa nina suala dogo sijui kama ninaruhusiwa kumuuliza ama vipi. Kama siruhusiki basi nitaomba nitaendelea kumjibu.

Kuhusiana na miche hii chenza jemu, pilipili doria na kila kitu ulivyovitaja Kizimbani haiko lakini katika nasari zetu ipo na tunakukaribisha kama ilivyo tunaomba uje na ununue, ipo katika Idara ya misitu inapatikana na kwa macho yangu mimi nimeiona na hivi sasa pia na mimi nina mpango na mimi pia nikaipande miti hiyo.Ahsante. (*Makofi*)

Nam. 84

Ujenzi wa barabara ya kutoka Kojifa hadi Bandarini kwa kiwango cha Lami

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:-

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuja kufungua soko la samaki na mboga mboga katika Jimbo la Tumbe, moja ya ahadi yake alisema ataijenga barabara ya kutoka Kojifa hadi Bandarini kwa kiwango cha lami na tayari ujenzi umeanza kwa kuweka kifusi lakini barabara hiyo inaanza kuchimbuka.

(a) Je, Wizara yako inalijua hilo la ahadi ya Mhe. Rais.

(b) Ni lini sasa barabara hiyo itakamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Wizara yangu inatambua ahadi ya Mhe. Rais ya kuijenga barabara hiyo katika kiwango cha lami.

(b) Wizara inaendelea kuifanyia matengenezo madogo madogo barabara hiyo hadi hapo fedha za kutia lami barabara hiyo zitakapopatikana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa barabara zilizomo kwenye ilani ya CCM, 2015/2020 ni barabara ya Fuoni-Kombeni, Kijitoupele-Mambosasa na ukizingatia barabara zile mpaka sasa hazijaanza ukarabai wa aina yoyote.

Je. Mhe. Waziri, ni lini serikali itaweza kuanza kujenga barabara hizo alau tu kwa kuweza kupita na kuitegeleza Ilani yetu kwa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama alivyosema barabara zile alizozitaja ziko

katika Ilani ya uchaguzi wa CCM na kwa upande wa Zanzibar kwamba tuliahidi tutajenga barabara zenye urefu wa kilomita 160.8 na sisi tunahakikisha kwamba ahadi hiyo tunaitimiza.

Sasa kwa upande wa barabara ya Fuoni - Kombeni, barabara hii ipo pamoja na barabara anayoiulizia sana Mhe. Nadir-Abdul-latif katika barabara zile zenye urefu wa kilomita 51 ambazo kupitia ufadhili wa *ADB* karibuni tunategemea kuzijenga. Kwa hiyo, mimi namuomba awe na subira barabara hizi kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutazijenga karibuni na barabara ile ya Mambosasa ile tunagetemea katika kipindi kijacho nayo tuweke katika vipaumbele vyetu vya Wizara katika kuijenga ili kuhakikisha kwamba Ilani ya uchaguzi wa CCM tunaitekeleza kwa vitendo na nina imani kubwa sana kupitia uongozi mahiri na shupavu wa Mhe. Dkt Ali Moh'd Shein, basi hakuna lisilowezekana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nimeshachoka kuwapa kauli wananchi wangu wa Jimbo la Chaani ambazo hazina meno kila siku wananiuliza sina la kuwajibu.

Ni lini Mhe. Waziri, barabara ya Chaani uwaahidi wananchi wanakusikia kwenye *TV* utaijenga?

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kumtoa wasi wasi kwamba barabara hii sasa hivi kama nilivyosema katika kikao chetu ya Bajeti katika barabara tuliyoitilia kipaumbele na hivi sasa tumeshaanza kulipa fidia kwa wananchi walioathirika au watakaoathirika na ujenzi huu. Kwa hiyo, mimi namuomba avute subira na katika kipindi cha karibuni kabisa tutapata mshauri elekezi na baadae mkandarasi wa kuijenga barabara.

Kwa hiyo, mimi namtoa ghofu aendelee kusubiri na wananchi wake na kama nilivyosema mwanzo kwamba kupitia Ilani ya uchuguzi wa CCM tutahakikkisha kwamba ahadi zote alizotoa Mheshimiwa Rais, kupitia ilani au yeye mwenyewe basi tunazitekeleza ipasavyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu wa maswali kwa mujibu wa kanuni umemalizika, lakini kwa kutumia kanuni ya 39, kifungu cha 3 tutaengeza dakika 15 kumalizia swali ambalo limebakia.

Nam. 132

Ujenzi wa barabara ya Mgelema

Mhe. Shaib Said Ali - Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar kwenye kampeni zake wakati wa kuomba kura kwa wanachi hutoa ahadi nyingi na wananchi hao na matumaini makubwa juu ya utekelezaji wa ahadi hizo. Moja kati ya ahadi hizo ni utengenezaji wa barabara ya Mgelema ilioko Jimbo la Chonga.

(a) Je, Mhe. Waziri, anawaambia nini wananchi wa Mgelema kwa kadhia wanayoipata ikiwa sasa ni awamu ya nne huwekewa ahadi hiyo.

(b) Je, Mhe Waziri, haoni kutokutengenezwa kwa njia hiyo kunasababisha zao la karafuu kuuzwa zaidi kwa njia ya magendo kutoka kijiji hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.132 kama ifuatavyo:-

Kwanza, nakubaliana na suala la Mhe. Mwakilishi kwamba, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitoa ahadi ya kuijenga barabara ya Kipapo – Mgelema na barabara nyengine mbili za Mgagadu – Kwautao na Uyuni -Ngomeni.

Barabara hizo tulipewa maagizo Wizara tatu, yaani Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa kuanzia tuliifanyia matengenezo barabara ya Uyuni – Ngomeni ambayo sasa hivi inapitika vizuri bila matatizo, aidha, tumefanya utaratibu wa kuijenga barabara nyengine inayoitwa Barabara Tau na barabara ya Kipapo – Mgelema nayo tunategemea kuijenga. Tunamuomba Mhe.Mwakilishi, avute subira kwani ujenzi wa barabara hiyo utaanza karibuni.

Mhe, Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Mgagadu – Kwautao ambayo ni ahadi ya Mhe. Rais, pia ilikuwa katika hali mbaya na karibuni tu tuliiweka *grader* na hivi sasa inapitika. Kwa hiyo, mauomba sana Mheshimiwa, azidi kuvuta subira na hiyo barabara tunamuhakikishia kwamba tutaitegeneza kupitia agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shaib Said Ali: Mhe. Mwenyekiti, njia ya Mgelema ni njia ambayo wananchi wana kilio kikubwa sana kwa sababu ni njia ambayo zao la karafuu ndiko linakotoka.

Je, ni lini basi Mhe. Naibu Waziri, njia hii itaanza kutengenezwa ili wananchi wapate kuitumia njia yao kwa hali ilivyo na itatengenezwa kwa kiwango cha lami au cha fusi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, lakini pia naomba radhi kwa sababu kulikuwa na swali (b) kuhusu swali lake alilouliza kwamba kutotengenezwa kwa barabara hiyo, je, hakusababishi kufanyika kwa magenzo ya zao la karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nataka kumtoa wasi wasi kwamba biashara au magendo ya zao la karafuu inatoka na utashi wa mtu mwenyewe na sio sababu barabara.

Pili, nataka kumuhakikishia kwamba barabara ile tutaijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali yatu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutengenezea barabara nzuri za Zanzibar ikiwemo Fuoni pamoja na barabara yangu ya Gando Wete.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika utengenezaji wa barabara hii ahadi ya Mhe. Rais, ni kuwalipa fidia wale ambao hawajalipwa majumba yao kabla ya kupitishwa barabara na baada ya upitishwaji wa barabara hii.

Lakini katika maswali yangu na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, ni kwamba utaratibu unaendelea kuchukuliwa ili kuwalipa wananchi hawa. Je, taratibu hizi zitamalizika lini na je, huoni Mhe. Naibu Waziri, ucheleweshwaji wa taratibu au malipo haya ni kuwakatisha tamaa wananchi wangu wa jimbo la Gando.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Waziri, kama nilivyolijibu katika swali lake alivyouliza hivi karibuni ni kwamba, wizara tunajua kwamba tunadaiwa sehemu tafauti ikiwemo barabara hii ya Gando - Wete na Gando - Konde pamoja na vile vile nilivyomjibu Mheshimiwa barabara zile za *Noral*.

Kwa hiyo, mimi karibuni tu nilikuwepo kule kwenye ziara nilitembelea maeneo tafauti na kukutana na watu wanaotaka kulipwa fidia ikiwemo Jimbo la Wingwi na hata hii barabara ya Ole Kengeja. Kwa hiyo, mimi naomba watustahamilie, lakini tumesema kwamba hivi sasa tunapojenga barabara yoyote kwanza tulipe fidia, ndio maana tumeanza kulipa fidia kama mnavyoona barabara hii ya Mkokotoni mpaka hapa Bububu kwa hiyo, na hizi kwa sababu kipindi kilichopita tulikuwa hatujafanya utaratibu huo, lakini tutahakikisha kwamba kila siku zinavyoenda tutapunguza hili deni tunalodaiwa mpaka tulimalize kabisa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016

(Kusomwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia amani na utlivu katika nchi yetu, uliotuwezesha kukutana katika Baraza hili na kuendelea kutekeleza jukumu letu la msingi la kikatiba la kutunga sheria kama ilivyoainishwa katika Sura ya Tano ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Pili, naomba kuchukuwa fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kufanikisha mswada huu wa Sheria mpya ya usimamizi wa fedha za umma kuweza kuwasilishwa katika kikao hiki.

Mhe. Mwenyekiti kwa namna ya kipekee kabisa napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya Biashara na Kilimo Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni. Pia, kwa Makamu wake Mhe. Hamida Abdalla Issa, pamoja na Wajumbe wote na Makatibu wote wa Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya kuupitia na kurekebisha kasoro zilizojitokeza wakati wa uchambuzi wa mswada huu. Napenda niwahakikishie kwamba michango yao tunaithamini sana na imezingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Said Hassan Said na watendaji wake wote kwa kuandaa mswada huu wa Sheria mpya ya Usimamizi wa Fedha za umma na kufanya tafsiri ya Kiswahili ninayoiwasilisha hapa.

Vile vile, namshukuru kwa dhati Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Ndugu Khamis Mussa Omar na Naibu Katibu Mkuu ndugu Ali Khamis Juma na watendaji wote wa wizara yetu waliohusika na uandaaji wa mswada wa sheria hii.

Aidha, naomba kuwashukuru sana uongozi wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara za SMZ na wote waliochangia kwa namna moja au nyengine katika uandaaji wa mswaada wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, pia, naomba kutambua mchango mkubwa uliotolewa na mamlaka ya uchapaji iliyo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kuchapisha kwa wakati mswada yetu yote tulioiwasilisha hapa Barazani katika kikao hichi kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, matayarisho ya Mswada wa Sheria mpya ya usimamizi wa fedha za umma yalifanywa kwa mashirikiano makubwa kutoka kwa washauri wa maswala ya usimamizi wa fedha katika kanda ya Afrika Mashariki na kati *IMF East Afrika*, Taasisi za Serikali na wataalam wengine waliobobea katika fani ya usimamizi wa fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha namba 12 ya mwaka 2005 kulibainika kasoro mbali mbali zikiwemo hizi zifuatazo:-

Kwanza, Sheria ya Fedha za Umma iliiopo, kutokujuisha usimamizi wa fedha na mali za umma katika serikali ya mitaa na mashirika ya umma.

Pili, Sheria ya sasa ya kutozingatia baadhi ya maeneo muhimu ya usimamizi wa fedha za umma kama vile utaratibu mzima wa uandaaji na usimamizi wa bajeti.
Tatu, Kupitwa na wakati kwa sheria inayosimamia mikopo, misaada, dhamana ya mwaka 1978 ambapo katika nchi nyingi dumiani maswala haya hujumuishwa moja kwa moja katika sheria ya fedha.

Nne, Sheria haikuweka bayana makujumu ya ngazi muhumu za serikali kama vile Baraza la Mapinduzi la Maofisa Wahasibu asili.

Tano, Sheria haikuhusisha maswala ya ukaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi. Kwa upande mwengine kumejitokeza upungufu katika mfumo wa kitaasisi ikiwemo usimamizi wa ukaguzi wa ndani kuwa chini ya Muhasibu Mkuu wa serikali.

Sita, Sheria ya usimamizi wa fedha iliyopo kutokenda sambamba na sheria nyengine zinazohusiana na usimamizi wa fedha za umma katika Ukanda wa Mashariki ya Afrika na kwengineko.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya mswada huu ni kufutwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2005 na Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana (*Loan Decree*) ya mwaka 1978, Sura ya Tano na kutunga Sheria mpya ya usimamizi wa fedha za umma itakayoweka misingi imara ya usimamizi wa fedha za umma. Mswada huu unakusudia kujumuisha maeneo muhimu ya usimamizi wa fedha za umma ambayo hayakujuishwa katika Sheria ya Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2005 na Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya mwaka 1978.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada pia umejikita zaidi katika eneo la kugawanya majukumu ya usimamizi wa fedha za umma katika ngazi tofauti za uongozi kwenye utayarishaji na utekelezaji wa bajeti, masuala ya ukadiriaji na ukusanyaji wa mapato, matumizi, usimamizi wa mali, usimamizi wa madeni, utayarishaji na uwekaji wa hesabu na ukaguzi katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu umegawika katika sehemu kumi na tano. Maelezo kwa ufupi juu ya sehemu hizo ni kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza:
Inahusu Masharti ya Awali ambayo inajumuisha jina fupi na kuanza kutumika Sheria, kuhusika kwa Sheria, Matumizi ya Sheria hii, Misingi ya usimamizi wa fedha na tafsiri ya maneno muhimu yaliyotumika ndani ya Mswada wa Sheria.

Sehemu ya Pili:
Inahusu Kazi na uwezo wa Baraza la Mapinduzi na watendaji wakuu wa Serikali.

Sehemu ya Tatu:
Inahusu Kuanzishwa kwa Hazina ya Serikali ambayo itajumuisha Waziri, kwa maana Waziri Anayehusika na Masuala ya Fedha, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Mhasibu Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wa Idara.
Sehemu hii pia itakuwa na majukumu ya jumla ya Serikali, majukumu maalum ya Serikali, uwezo na majukumu ya Waziri, Mlipaji Mkuu wa Serikali na uwezo na majukumu ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Sehemu ya Nne:

Inahusu Mfuko Mkuu wa Hazina Mifuko Maalum. Sehemu inayozungumzia uwepo wa Mfuko Mkuu wa Hazina kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya 1984, Kifungu cha 104.

Sehemu ya Tano:
Inahusu Dhamana ya Maafisa Wahasibu, Kazi za Maafisa Wahasibu zinazohusiana na masuala ya usimamizi wa fedha yakiwemo masuala ya kibenki, usimamizi wa fedha za umma, usimamizi wa mali, madeni, mapato na matumizi pamoja na utayarishaji na uwasilishaji wa bajeti.

Sehemu ya Sita:
Inahusu uandaji wa mipango na uidhinishaji wa bajeti. Kuimarisha misingi ya uwajibikaji wa kifedha, Hazina ya Serikali kuandaa mpango wa bajeti, misaada na mikopo, maandalizi ya bajeti pamoja na kuidhinishwa na kupitishwa kwa bajeti kuu ya Serikali.

Pia, sehemu hii inazungumzia matumizi ya fedha kabla ya kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Sehemu ya Saba:
Inaelezea utekelezaji wa bajeti kuu ya Serikali pamoja na masharti yake.

Sehemu ya Nane:
Inahusu kuanzisha Mfuko wa dharura *(Emergency fund)* ambayo umeelezwa ndani ya Katiba ya Zanzibar Kifungu cha 108. Mtaji wa mfuko huo na matayarisho na uwasilishaji wa marekebisho ya bajeti ya mwaka ya mfuko.

Sehemu ya Tisa:
Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii inahusu masuala ya benki na usimamizi wa fedha na inajumuisha kuwepo kwa utaratibu wa kibenki, usimamizi wa fedha taslimu. Pia, kumetolewa maelekezo ya ufunguzi wa hesabu za kibenki kwa taasisi za Serikali ambapo Mlipaji Mkuu wa Serikali ataruhusu ufunguzi wa hesabu hizo.

Sehemu ya Kumi:
Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii inahusu kukopa, kukopesha na usimamizi wa madeni ya Serikali. Sehemu hii inazungumzia mamlaka ya kukopa kwa niaba ya Serikali, taratibu zitakazotumika katika ulipaji na ukopeshaji, kiwango cha kukopa na kiwango kitakachoruhusika kukopwa. Aidha, sehemu hii imezungumzia uwekaji bora wa kumbukumbu za madeni pamoja na uandaaji wa sera za madeni.

Sehemu ya Kumi na Moja:
Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii inazungumzia usimamizi wa fedha za umma katika Serikali za Mitaa ambapo Sheria imeelezea uanzishwaji wa jukwaa la bajeti na uchumi, kazi za Mabaraza katika masuala ya usimamizi wa fedha za umma, uwezo wa kukasimu kwa kazi ya Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa na Afisa Mhasibu katika Serikali za Mitaa, mapato ya Serikali za Mitaa, mikopo na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inayopokelewa katika Serikali za Mitaa.

Sehemu ya Kumi na Mbili:
Mhe. Mwenyekiti, inazungumzia usimamizi wa fedha za umma katika Mashirika ya Umma ambapo Mswada umeainisha kwamba Bodi za Mashirika zitakuwa ni chombo kitakachowajibika kufuata Sheria hii. Pia, inazungumzia masuala ya bajeti na mipango ya mashirika ya umma, utekelezaji wa bajeti na ufuatiliaji uwasilishaji wa ripoti za mwaka kiutendaji na kifedha.

Sehemu ya Kumi na Tatu:
Mhe. Mwenyekiti, inahusu uandaaji na uwasilishaji wa ripoti za utekelezaji za mwaka, ukaguzi na usimamizi wa kina katika masuala ya fedha, uanzishwaji wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani, Kamati za Ukaguzi, miongozo ya kutumia viwango vya kimataifa katika kufunga mahesabu, kutayarisha na kuwasilisha ripoti za mwaka za hesabu, kukaguliwa kwa hesabu za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na uwasilishaji wa ripoti za hesabu za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Sehemu ya Kumi na Nne:
Mhe. Mwenyekiti, inahusu masuala ya adhabu zitakazotolewa kutokana na kutofuatwa kwa taratibu za kifedha.

Sehemu ya Kumi na Tano:
Mhe.Mwenyekiti, sehemu hii na ndiyo ya mwisho inazungumzia masharti ya jumla ikiwemo kutungwa kwa Kanuni na kufutwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Nam.12 ya 2005 na Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya 1978, Sura ya 5 na kubakiza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kueleza kwamba Mswada wa Sheria unaowasilishwa umelenga kuimarisha Sheria kwa kutatua matatizo yaliyojitokeza kwa kuzipa uwezo taasisi za Serikali na watendaji, kushurutisha kutumika kipimo cha taaluma *(Best practice and professional standard)* katika usimamizi wa fedha na udhibiti wa raslimali za umma.

Vile vile, kuhakikisha unakuwepo uwazi, uwajibikaji na usimamizi madhubuti wa mapato, matumizi, mali na dhima katika taasisi za umma.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo)

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nitoe Hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kudhibiti na Usimamiaji wa Fedha za Umma na kuweka mambo mengine yanayohusiano hayo na Kufuta Sheria ya Usimamizi ya Fedha za Umma ya Nam. 12 ya 2005.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataalla* kwa kutujaalia uhai na uzima na tukaweza kuonana tena katika Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Aidha, nachukuwa fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kuweka Masharti Bora na Kufuta Sheria Usimamizi ya Fedha za Umma Nam. 12 ya 2005.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inatoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona kuwa sasa kuna umuhimu mkubwa wa kuifanyia marekebisho Sheria hii iliyopo ili iendane na wakati tulio nao kwa lengo la kuimarisha na kuweka misingi imara katika kusimamia Fedha za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Wizara ya Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed, Katibu Mkuu wa Ndg. Khamis Mussa pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano makubwa waliyoipa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo katika kipindi chote cha kupitia Mswada huu hadi leo hii tunausoma katika Baraza lako tukufu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, lengo la kuletwa kwa Mswada huu ni kufuta Sheria iliyokuwepo na kuandika Sheria mpya kwa lengo la kuweka misingi bora ambayo itaendana na wakati tulionao na mahitaji

yaliyopo. Mswada huu mpya unaanzisha Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani ambapo katika ile Sheria ya awali haikuwemo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwepo masharti yaliyowekwa Kikatiba katika kifungu cha 104 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na masharti yaliyoelezwa katika Mswada huu, katika kifungu cha 20 ambapo yanatambua kuwepo kwa Mfuko Mkuu wa Hazina ambao mapato yote ya Serikali, mikopo ya ndani na nje na misada inayopelekwa Serikalini yanatakiwa kuwekwa katika Mfuko huu. Jambo hili ni zuri sana kwani unakuwepo udhibiti bora kwa fedha zote za umma kwa sababu ipo mfuko mmoja.

Lakini pamoja na masharti hayo, bado kuna tatizo kubwa sana katika Mifuko Maalum inayoanzishwa kwa mujibu wa Sheria au anayoianzisha Waziri kwa mamlaka aliyopewa. Mfano wa Mifuko hiyo ni Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Miundombinu, Mfuko wa Maafa, Mfuko wa Madawati, nakadhalika. Pamoja na mifuko hii kuwekewa vianzio vyake vya uhakika, lakini bado kuna tatizo kubwa sana la upatikanaji wa fedha zake kwa wakati na kufanya mifuko hii kutokutekeleza kazi zake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linatakiwa kuangaliwa kwa umakini mkubwa sana, kwani ipo Mifuko mingi iliyoanzishwa lakini utekelezaji wake bado ni wa kusuasua, Kwa hivyo, Kamati yangu inamuomba sana Mhe. Waziri, ambaye ndie msimamizi mkuu wa Sheria hii kuhakikisha kuwa Mifuko yote inayoanzishwa ahakikishe kuwa fedha za mifuko hiyo zinapatikana kwa wakati na vile vile ahakikishe kuwa fedha hizo zinatumika kwa matumizi yale tu yaliyokusudiwa na si vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Mswada huu katika kifungu cha 54, unaanzisha Mfuko wa Dharura. Uanzishwaji wa Mfuko huu ni muhimu sana katika nchi yetu kwani yapo baadhi ya mambo ambayo hutokezea na kulazimisha fedha za umma zitumike pasi na kufuata utaratibu unaokubalika kisheria kwa mfano, maafa, maradhi ya mripuko na kadhalika. Lakini katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki ambacho kinamruhusu Waziri kutanguliza fedha za matumizi kwa mujibu wa utaratibu na baadae kuomba idhini ya Baraza la Wawakilishi juu ya matumizi hayo. Kwa mnasaba huo, Waziri atatumia fedha kwanza na baadae ndio Baraza linaidhinisha, lakini suala linakuja je, vipi ikitokea Baraza halikuidhinisha matumizi haya na fedha wakati huku zimeshatumika? Kamati inaomba sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliangalie eneo hili kwa hadhari kubwa ili itakapotokea hali hii basi busara itumike zaidi kwa matumizi ya fedha za umma kwa mazingira hayo niliyoyaeleza hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu umekuja na mapendekezo mazuri ya Usimamzi wa fedha katika Serikali za Mitaa, Wajumbe wa Baraza hili watakuwa mashahidi kuwa Serikali za Mitaa zinakusanya na kutumia fedha nyingi za wananchi kwa ajili ya maendeleo katika maeneo husika. Lakini usimamizi uliobora unahitajika ili kuhakikisha fedha hizi zinasimamiwa ipasavyo. Katika Mswada huu, Waziri wa Fedha kwa kushauriana na Mabaraza ya Serikali za Mitaa ataanzisha Jukwaa la Bajeti na Uchumi, lengo kubwa la jukwaa hili ni kuweka utaratibu wa mashauriano yatakaotumiwa na Waziri wa Fedha, Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kuhusiana na masuala ya fedha za Serikali ya Mitaa na mahusiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kuhusu utaratibu na mipango ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu pia umeweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa fedha katika Mashirika ya Umma, tunamuomba sana Mhe. Waziri, awe muangalifu sana juu ya usimamizi wa fedha katika Mashirika ya Umma kwani zipo dalili nyingi kwa baadhi ya Mashirika ya Umma kutokuwa na usimamizi mzuri wa fedha wakati wa kukusanya na kwa matumizi ya fedha hizo. Hivyo, Mhe. Waziri, atakuwa shahidi kuwa, endapo Mashirika ya Umma hasa yale yanayojiendesha kibiashara na kutoa huduma moja kwa moja endapo hayatokuwa na usimamizi mzuri wa kifedha ni wazi tanaweza kupoteza mwelekeo na kusababisha mzigo mkubwa kwa Serikali na wananchi kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kuwa, usimamizi wa Fedha za Umma katika Serikali kuu upo katika Mfuko Mkuu wa Hazina, hii ni sehemu muhimu sana ambayo inahitaji usimamizi wa hali ya juu katika kuhakikisha kuwa fedha zinazotoka katika Mfuko kwa ajili ya matumizi zinatumika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Kamati yangu inamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali ambaye ndiye Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa Mfuko huu unasimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa Sheria.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukuwa nafasi hii kumkumbushe Mhe. Waziri, kwa mujibu wa masharti ya Mswada huu kuna baadhi ya taarifa zilizoelezwa ambazo zitahitajika kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi, tunaomba sana taarifa hizi ziwasilishwe kwa wakati na kama zilivyoelezwa katika Mswada huu. Kamati yangu itaendelea kumkumbusha Mhe Waziri juu uwasilishwaji wa taarifa hizi mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kuweka uwazi na uwelewa kwa wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimkumbushe tena Mhe. Waziri pamoja na Sheria nzuri zenye masharti mazuri tunazozitunga hapa Barazani, lakini kama hatutakuwa na usimamizi mzuri wa Sheria hizi bado tutakuwa hatujafanya kitu kwani wapo baadhi ya watendaji ambao sio waadilifu katika kutekeleza majukumu yao. Kwa hivyo, wakati wa utekelezaji wa Sheria hii tunakuomba sana usimamizi sheria hii isimamiwe vizuri kwa lengo la kuweka usimamizi bora katika fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla, Kamati yangu iliupitia Mswada huu kifungu kwa kifungu na kufanya baadhi ya marekebisho kama yanavyoonekana katika nakala ya marekebisho ambayo Wajumbe mumepatiwa. Marekebisho haya yalizingatia makosa ya kilugha, tafsiri baina ya nakala ya Kiswahili na Kiengereza pamoja na marekebisho ya msingi ambayo yaliboresha Mswada huu. Miongoni mwa marekebisho ya msingi yaliyofanywa na Kamati ni kama yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 16 ambacho kinaanzisha nafasi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imependekeza kuweka sifa za Mhasibu Mkuu wa Serikali, sifa hizi zimeainishwa katika nakala ya marekebisho ya Kamati. Vile vile, katika Mswada huu, Sehemu ya Kumi na Tatu ambayo inaanzisha nafasi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani, Kamati yangu pia ilipendekeza kuweka sifa za Mkaguzi huyu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa uvumilivu wao hadi kufanikisha kuupitia Mswada huu, kwa sababu kazi haikuwa rahisi. Sasa niruhusu niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa majina kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ussi Yahya Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	Mjumbe
5.	Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	Mjumbe
6.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe
7.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
8.	Ndg. Salum Kamis Rashid	Katibu
9.	Ndg. Asma Ali Kassim	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na usikivu wa hali ya juu waliouonesha wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii fupi. Niwaombe sana kuupitia kuujadili kwa kina na hatimae kuupitisha Mswada huu wa Usimamizi wa Fedha za Umma ili Mhe. Waziri, apate kutekeleza Sheria hii.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa uwasilishaji wenu na mimi pia niungane nanyi kuwapongeza katika kuwasilisha hotuba yenu hii.

Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji nilionao ni wanne mpaka sasa. Kwa hivyo, naomba nimwite mchangiaji wa kwanza Mhe. Machano Othman Said, ili naye kuchangia Mswada huu na wa pili atafuata Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kuweza kuchangia Mswada huu wa fedha. Pili, naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, na mpongeza pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara yake na timu yao yote, kwa hakika tangu juzi tunasema kwamba ni kazi kubwa wamefanya, leo nafikiri ni siku ya tatu mfululizo tunapokea na kujadili na hatimaye kupitisha Miswada ambayo inasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hii inaonesha kwamba watendaji wa wizara hii wamejifungia na kufanya kazi nzuri ambayo inaleta tija kwa nchi yetu.

Aidha, nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, pamoja na wajumbe wake kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa niaba ya Baraza letu la Wawakilishi. Kwa hakika wamefanyakazi kubwa Miswada hii ni mirefu na imewachukulia muda mwingi wa kufanya kazi kwa umakini, na leo tunahitimisha mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia huu mswada nitachangia baadhi ya vifungu, vifungu ni vingi sana Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi nataka nianze na kifungu cha 8. Tukisoma katika kifungu cha 8 ni;

"Kunaanzishwa taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakayojulikana kama Hazina ya Serikali".

Katika kifungu hiki cha mswada huu wa sheria unaelezea Hazina ya Serikali itajumuisha;

a) Waziri ambaye atakuwa mkuu wa hazina;
b) Mlipaji Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Hazina;
c) Mhasibu Mkuu wa Serikali; na
d) Wafanyakazi wa Idara au Ofisi za Hazina za Serikali zinazohusika na fedha na masuala yanayohusiana na fedha.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nije katika kifungu cha (d). Inawezekana ndio lengo lake au pengine sio lengo lake. Lakini Mhe. Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho atatuambia. Kwa utaratibu wa serikali, washika fedha wote ambao wameajiriwa na serikali wanakuwa chini ya Hazina au chini ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, hata kama yuko katika taasisi nyengine ya serikali, yuko wizara ya serikali, lakini anakua katika mamlaka ya wizara ya fedha au tuseme Hazina. Sasa sijui kama hiki kifungu cha (d) ndio kinawajumuisha na wao au kinajitosheleza kwa suala hili na kama hakijitoshelezi basi tuangalie namna ya kuwaweka na wao watambulikane.

Mhe. Mwenyekiti, najua uko utaratibu mzuri wa serikali wa kuwapanga hawa washika fedha, kwa sababu washika fedha ni watu muhimu sana katika kusimamia matumizi ya serikali. Kwa hivyo, tuangalie na utaratibu ambao upo wa kuwasimamia na kuwaelekeza la kufanya katika majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia, kuna kifungu cha 10 cha mswada huu wa sheria ambacho kinasema,

Kifungu cha 10;

"Majukumu maalum ya Hazina ya Serikali"

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu kwa ninavyohisi mimi ni kuona rasilimali ya fedha inatumika vizuri kwa manufaa ya taifa, ndio lengo kuu la Hazina, kwamba rasilimali inayokusanywa basi iweze kutumika vizuri kwa ajili ya maendeleo yetu. Lazima tukiri kwamba Awamu hii ya Saba, Sehemu ya Pili sasa imeanza vizuri katika kukusanya rasilimali ya taifa. Mhe. Rais, tunamshukuru na kumpongeza, lakini pia tumpongeze na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kusimamia majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, tulichelewa kidogo kuanza na tulipoanza baada ya uchaguzi wetu wa marejeo Wapinzani wetu wengi walikuwa wanasema aah! Serikali ile itaishia njiani, haina pesa hata ya mishahara. Lakini nafikiri wameona wenyewe kwamba mishahara inatoka, na sio mishahara tu, sisi wajumbe wa kamati ambao tumetembelea taasisi za serikali, kwa mara ya kwanza tumekuta *OC* wanapata zaidi ya asilimia 80 au 90, huwa sio jambo la kawaida kwa *OC* kupatikana kwa kiwango hicho, kwa kawaida huwa tunapata mishahara kwa asilimia mia, lakini wakati mwengine ilikuwa *OC* asilimia 15, 20 mpaka 40. Lakini sasa *OC* inakwenda mpaka sehemu nyengine tumetembelea asilimia 100 *OC* wamepata.

Kwa hivyo, haya tunasema ni majukumu ya Hazina kwamba rasilimali ya fedha au rasilimali fedha inatumika vizuri katika ugawanaji wa mamlaka ya nchi yetu na kuwapatia tija wananchi. Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, nataka nichomekee, sisi Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wengine huwa tunaitikia sana wito wa serikali katika kufanya mambo ya kuleta maendeleo. Sasa hivi Waheshimiwa Wawakilishi kwa umoja wetu tulikubaliana na wazo la serikali la kuchangia madawati, nafikiria mchango unakwenda vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, ninaloliomba ukishamaliza ule muda wa kuchangia basi serikali itafute wajenzi wa madawati watakaotufanyia kwa bei nafuu, kwa sababu na wao watakuwa wanatoa sadaka kwa upande mmoja, isiwe tena humo ndani mna *percent*, halafu sasa baada ya kupatikana madawati, katika ugawanaji wa madawati, katika mgao ule na Waheshimiwa Wawakilishi, nao washirikishwe vizuri ili kuhakikisha kwamba yanafika katika maskuli yao na yanakuwa yako katika usalama vizuri, ili wakatowe elimu kwa wananchi kwamba yale madawati yanatakiwa kutunzwa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kwa Hazina kushirikiana na *BoT* katika kuweka Sera za kifedha katika uwekezaji wa fedha za serikali na mashirika ya umma katika benki mbali mbali. Sina uhakika na utaratibu wetu wa sasa, lakini wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wamekuwa na sera zao kwamba serikali lazima iwekewe katika benki ya *BoT*, hapa kwetu tunaweka kwenye benki ya *PBZ* au vipi, sijui utaratibu huu ukoje, pengine Mhe. Waziri, atatueleza kwa kupitia mswada huu wa Sheria ya fedha, kwamba taasisi za serikali sio lazima ziwe zinapata maelekezo ya uwekaji wa fedha wapi waweke, kwa misingi gani na kwa faida ya serikali na gawio la serikali linakuaje. Hilo naomba pia Mhe. Waziri, aje atufahamishe.

Mhe. Mwenyekiti, pia, jambo jengine la msingi ni kulinda Mfuko Mkuu wa Hazina. Humu katika mswada umeelezwa Mfuko Mkuu wa Hazina maana yake

na mifuko maalum maana yake. Nimeona, nafikiri kifungu hiki kwamba haitakiwi Mfuko wa Hazina uwe hauna kitu, kila wakati lazima uwe umenonanona hivi. Kwa hivyo, serikali kwa kupitia kwa Mkuu wa Hazina ambaye atakuwa ni waziri, basi tujuwe kwamba tuna wajibu wa kulinda Mfuko wetu wa Hazina ili uweze kuwa vizuri.

Vile vile, kuandaa mfumo wa taasisi za umma kukopa au kuingia katika madeni. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo jema sana ambalo limo katika mswada huu. Kulikuwa na taratibu baadhi ya taasisi za umma na zaidi kwa mikopo ya ndani walikuwa hawashirikishwi sana Wizara ya Fedha. Mtu anakwenda anazungumza akiona mkopo upo anajichukulia, lakini wakati wa ulipaji wa deni lenyewe unakuwa ni mzigo wa Serikali Kuu. Kwa hivyo, sasa kwa ajili hiyo kwamba kutakuwa na utaratibu wa kuandaa mfumo ambao utakuwa kila mtu anauelewa, na taasisi zote zitakuwa zinauelewa, kwamba ukitaka kukopa fedha basi ni lazima ufuate utaratibu huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninalo pendekezo hapa katika kufanya kwamba mambo yaende vizuri ya serikali, zipo baadhi ya taasisi za serikali zinapewa ruzuku katika uendeshaji wake. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, wawe na timu ya uhakika ya kuhakikisha kwamba kweli hizi taasisi haziwezi kujitegemea. Tunapozunguka huko tunakuta taasisi zile ambazo zinapewa rukuzu mapato yao yanashuka na kwa sababu wanajua kwamba sisi ukifika mwisho wa mwezi Hazina itatupa ruzuku hii. Kwa hivyo, na wao mapato yao ama kwa makusudi au kwa kutokufanya kazi kwa bidii mapato yanashuka, lakini ukiwapa kazi kwamba mfike asilimia hii ndio mpate hiki kidogo, nafikiri mambo yanaweza kuwa mazuri na kuongeza mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie Sehemu ya Sita kuhusu uandaaji wa mpango, bajeti na uidhinishaji wa bajeti ambayo inazungumziwa na kifungu cha mswada huu, kifungu cha 37, 38 na 39 kwa pamoja. Kwanza nimpongeze tena Mhe. Waziri na serikali kwa jumla kwa makusanyo mazuri ya mapato. Wametoka kwenye makusanyo ya asilimia pengine kwenye bilioni sijui 30 mpaka karibu 50, kwamba haya ni juhudi zao. Lakini pia nirejee tena kuwapongeza kwa ugawanaji mzuri wa hiki ambacho kinapatikana, ikiwemo *OC*, mishahara na mambo mengine. Lakini pia ulipaji wa madeni ya ndani ikiwemo viinua mgongo na kuwapa watu pencheni zao kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo halina budi kupongezwa sana na Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kwamba wakati wa uandaaji wa bajeti, kama ambavyo imeelezwa katika utaratibu wa mswada huu na sheria hii, kwamba ni

muhimu na lazima wadau wote washirikishwe mapema. Kwa mfano, bajeti ya mwakani ya mwaka 2016/17, sasa tunakwenda tena kwenye bajeti ya 2017/2018. Sasa tuandae mapema, vipaumbele vyetu wale wadau wetu au washirika wa maendeleo wajuwe mapema, kama kasoro watowe mapema ili itowe nafasi kwa serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuona kwamba je, yale mapendekezo yao yana mantiki au yakoje na yatafanywa nini, ili kuondoa malalamiko ya wananchi.

Sehemu ya Kumi, Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumzia pia kukopa, kukopesha na usimamizi wa madeni. Kifungu cha 58(2). Mikopo ya nje. Katika kifungu hiki cha 58(2), Mhe. Waziri, kwa kupitia mswada huu ametueleza kwamba mikopo yote ya nje itaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Sasa mimi nilikuwa naomba tu maelezo ya ziada hapa Je, itakuwa ni ule wakati wa bajeti ambao ametuambia kwamba watakopa hapa na hapa au kutakuwa na utaratibu maalum ambao utashirikisha Baraza kuelezea taratibu za mkopo ili Baraza litowe idhini. Kwa hivyo, hapa nilitaka kujua tu na Mhe. Waziri, naomba baadae utakapokuja kwenye majumuisho unijibu kuhusu hili jambo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, Sehemu ya Kumi na Moja, usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri na mimi napongeza sana suala hili. Kwa sababu tumeshapitisha Sheria ya Serikali za Mitaa, yaani halafu kwa kuwa na uchakachuaji wa Madaraka Mikoani. Serikali za Mitaa kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ni taasisi ambazo zitatumia fedha nyingi, ni taasisi ambazo zitakuwa zimepewa majukumu ya kukusanya pia fedha nyingi za serikali. Ninaloliomba kwa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa kushirikiana na waziri muhusika wa Tawala za Mikoa. Kwanza kuzijengea uwezo hizi taasisi za Serikali za Mitaa, baadhi yake taasisi hizi nyingi yao bado hazina uwezo, lakini pia watendaji hawana waliokuwa wengi wenye utaalamu, zaidi kwenye sehemu ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya Halmashauri na Serikali za Mitaa, hadi leo washika fedha wao hawajaajiriwa na serikali. Unamkuta Afisa Mapato wa Serikali za Mitaa, Halmashauri hadi leo hajaajiriwa, yeye ndiye mwenye dhamana ya kwenda kukusanya mapato. Sasa tujiulize watu kama hawa kama hawajaajiriwa watakuwa na dhamana gani ya maisha yao, halafu uwape jukumu la kukusanya mapato.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tukipitisha sheria hii, nakuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kushirikiana na Serikali Kuu, pengine katika utumishi wa umma, Serikali za Mitaa, hawa watu wengine wana uwezo, wana uzoefu na wamefanyakazi kwa muda mrefu, waajiriwe ili waweze

kuiamini serikali na serikali iweze kuwaamini wao. Lakini pia itakuwa ni tija kwa kuongeza mapato ya nchi, hasa katika utaratibu mpya huu ambao tunauanza wa kupeleka madaraka mikoani, ambao utahitaji kuwa na wasimamizi na wataalamu endelevu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, tunaomba sana Serikali hizi za Mitaa, tuzilee, tuzisaidie na pia kuziunga mkono katika majukumu yao ya maendeleo.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba mswada huu nauunga mkono kwa asilimia mia, na kwa vile unafuta ile Sheria ya mwaka 2005 ya Usimamizi wa Fedha, basi Waheshimiwa Wawakilishi, tujitahidi tuupitie huu mswada, tuuchangie lakini baadae tuunge mkono ili tuone taratibu nyengine za kifedha zinakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa nilikuwa nafikiria pia sijui kama itawezekana katika mswada huu, serikali itowe Hazina iwe na sera kuhusu mabenki na mikopo na zaidi kwa wafanyakazi. Hakuna watu ambao wanakopeshwa ambao wana uhakika wa kulipa kuliko wafanyakazi wa serikali, kuliko wafanyabiashara na kuliko nani, kwa sababu mfanyakazi wa serikali kila mwezi akipata mshahara wake anakatwa. Kwa hivyo, kumuwekea riba ya kuanzia 18 au 20 huko ni kumuumiza sana na hali ngumu hii ya uchumi. Kwa hivyo, ningeomba pengine Hazina kwa kushauriana na *BoT*, angalau ingekuwa kwa wafanyakazi riba yao kuanzia asilimia 10, 12 au 14 hapo ingekuwa muafaka sana.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nikae kitako na kuunga mkono mswada huu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said wa Jimbo la Mfenesini kwa mchango wako. Sasa namuomba Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, akifuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, na kuweza kuchangia mswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii ya fedha, kwa usimamizi wao mzuri kuhakikisha kwamba serikali yetu inazidi kupata mapato kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mwenyekiti wa kamati pamoja na wajumbe wake wote, kwa juhudi na kazi kubwa waliyofanya na kupitia wadau mbali mbali kutuletea mswada huu ambao ni muhimu kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri na ahadi ya fedha zinakaa vizuri bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba sheria hii ni nzuri na imekuja wakati muafaka, hasa tukizingatia kwamba ni kitu ambacho kikitungwa huwa kinaleta manufaa na utaratibu mzuri wa kudhibiti kile kinachoelekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kijumla mimi niseme kwamba Mhe. Waziri, kwa kupitia wizara ihakikishe kwamba azma yangu ile ile wanatoa mfunzo kwa maafisa wa fedha, ili kuwe na udhibiti na usimamizi mzuri katika shughuli zao za kila siku. Mhe. Mwenyekiti, elimu au mafunzo kwa sehemu yoyote ile ndio njia moja wapo ambayo inaleta uhai na uelewa katika shughuli zao. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, suala la fedha ni suala la roho ya nchi na suala la fedha ni uhai wa kila mtu anayekaa katika nchi hii kuwa huduma itamjia kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda vizuri katika sheria zetu hizi za fedha na mambo yetu yatakwenda vizuri. Kuna mambo mengi ambayo serikali inajitahidi, hapa katika wizara zote zilizokuwemo humu katika Baraza hili wizara 13 zinamtegemea Waziri wa Fedha na Mipango. Kwa hivyo, mimi naomba pawe na mashirikiano mazuri kwa watendaji wetu hawa na kuhakikisha kwamba kila eneo au kona inayoguswa basi fedha zake ziwe zinasimamiwa vizuri na zinapatikana kuendesha mambo ya nchi yetu, kama; Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji yuko hapa, Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tunampigia kelele kila siku, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na mawaziri wote. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali haisemeki, yaani kila Wizara inaitegemea Wizara ya Fedha, kwa hivyo mimi naomba tu Mhe. Waziri, bado watoe mafunzo mazuri kwa kila sehemu, kila panapo mapato ya Serikali au makusanyo yoyote ambayo taaluma yake ipewe usimamizi mzuri wa matumizi yale.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ningemuomba sana Mhe. Waziri kiko kifungu kinachosema kuanzishwa kwa mfuko wa dharura, mimi nakubaliana na hilo kwa sababu kuna majanga mbali mbali yanatokea duniani au katika nchi yoyote ile, lakini kwa hapa kwetu na kwengineko, hakuna mtu anayemuombea mwenziwe baya atakuwa huyo hana akili timamu. Niseme tu kwamba tumuombe Mwenyezi Mungu haya majanga yasitufike katika nchi yetu, kwa sababu janga linapoingia au linapotokea huwa hulitegemei.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tu kwamba mfuko wa dharura kwa ajili ya majanga mbali mbali huu uwepo, kwa sababu unakuja katika wakati ambao hautarajiwi, lakini tunamuomba Mwenyezi Mungu hapa kwetu kama nilivyotangulia kusema yasitokee.

Mhe. Mwenyekiti, katika mambo yote unayoweza kujifanyia lakini hutegemei kusema naweka bajeti hii labda nitapata majanga fulani, pale Serikali inapotokea ndio haina budi lakini ikijiwekea kidogo kidogo basi inakuwa na hakiba ya kutosha na mfuko huu unaweza kutusaidia pindi linapotokea, tunamuomba Mwenyezi Mungu asituletee janga katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mfano kuna majanga ya kipindupindu, kuna majanga ya mafuriko katika maeneo yetu kama sisi wengine katika majimbo yetu ya Wilaya ya Magharibi (A) na (B) huwa ndio tuna kilio kikubwa zaidi, huwa watu wetu hawajielewi wanaelekea wapi. Kwa hivyo nasema mfuko huu utawasaidia watu wetu kwa wale wanaopatwa na maafa hayo lakini Mungu asituletee, tunaita hakiba haiozi.

Mhe. Mwenyekiti, mabaraza au kuanzishwa kwa Baraza la Bajeti katika Serikali za mitaa hili ni suala muhimu, na Serikali za mitaa zitajua vipi bajeti zao na mambo yao, lakini kubwa tu nitakaloliomba hapa au nitakalomuomba Mhe. Waziri juu ya uhaulishaji wa fedha, Serikali za mitaa zinahitaji Serikali kuu na matumizi yake yote yanategemea yatatoka katika Serikali kuu, kwa hivyo fedha zinapotoka hapa kwenda kwengine uhaulishaji wake tunategemea utatusaidia katika kutekeleza yale yanayoelekea katika Serikali za Mitaa na si vyenginevyo.

Kwa hivyo hapa pia nimuombe Mhe. Waziri kuwe na mahusiano mazuri kwa lengo la kujenga, kwa sababu sisi sote wajumbe hapa wa Baraza la Wawakilishi tuna Serikali zetu za mitaa, na kubwa likitokezea nitakimbilia huko kwanza kabla sijamfikia Waziri, Waziri atakuwa mtu wa mwisho kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la sheria hii ni kuanzisha miongozo ya sheria na taratibu za usimamizi wa fedha, Mipango na Makadirio. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri haya malengo ni mazuri kwa matumizi yake na malengo haya yatatusaidia na yatamsaidia yeye kujua kila aina ya taasisi au katika halmashauri zetu kuna tatizo gani lifanywe nini, yeye atakuwa kama ndio mkombozi wa mambo haya, baada ya kukusanya huko kote hapa panatakiwa hichi na hichi.

Jengine ninalomuomba sana Mhe. Waziri, Serikali ihakikishe hawa maafisa wa fedha wana sifa stahiki ili kuleta ufanisi mzuri wa sheria hii, naamini kila mtu ana fani yake na fani yako ndio utakayotumia kwa busara zako, kwa mfano tuna wataalamu hapa wa kilimo, madaktari, walimu na wengineo. Sasa fani ya watu wetu hawa maafisa wa fedha ni kuhakikisha wanafanya kazi zao vizuri kwa ajili ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Nimuombe sana Mhe. Waziri maafisa wa fedha wawe na sifa nzuri za stahiki zao katika ufanisi mzuri wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia nitamuomba Mhe. Waziri ahakikishe anatangaza Kanuni hizi ili utekelezaji wake wa sheria hii uwe mzuri zaidi, unapoweka sheria kuna kanuni zetu na sisi tunatunga sheria mbali mbali lakini katika Baraza hili kuna kanuni, kwa hivyo Mjumbe anatakiwa kanuni zake azielewe. Kwa hivyo na wenzetu hawa waelewe kanuni zao wanafanya nini kwa maslahi ya utekelezaji wao mzuri na kuleta ufanisi katika shughuli zetu za kila siku.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia kama Mjumbe Mwenzangu Mhe. Machano Othman Said kanifilisi, maana yake anayekutangulia wakati mwengine anakufilisi, na mimi kanifilisi lakini *point* nilikuwa nayo kubwa sana tunaingia katika shughuli hizi kwenda sambamba na Serikali zetu za mitaa, lakini kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, asilimia kubwa au unaweza kusema asilimia 80% wanaokusanya mapato katika Serikali za Mitaa hawajaajiriwa, kwa hivyo unapompa mtu kitu anasema mimi hapa madhali sijaajiriwa nachukua changu kidogo, udanganyifu utakuwepo.

Nimuombe sana Mhe. Waziri kwa kuwa tunakwenda katika Sheria mpya hii ambayo ni ya udhibiti wa Fedha za Umma pawe na haja, au pawe na rai ya makusudi kuwatafutia utaratibu wa kuwaajiri wafanyakazi wetu hawa wa Serikali za Mitaa Unguja na Pemba, tunaamini ukiwa katika Sheria umeajiriwa na utakapokuwa hujaajiriwa kuna mambo mawili tofauti, kwa sababu wewe unakikusanya lakini unaona hichi kikubwa kitakwenda kwa walioajiriwa mimi nitakikosa, sitegemei yatokee hayo, lakini natoa kama indhari tu. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hapo mbele katika bajeti ijayo watafute njia yoyote hawa wakusanyaji wetu wa mapato wote na wengineo waliokuwa hawajaajiriwa ambao wanafanya kazi nzuri katika Serikali za mitaa basi waajiriwe ili wawe katika orodha ya wafanyakazi katika Serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele, kwa kuwa Sheria hii ni ya Fedha zetu za Umma tunaiunga mkono au naunga mkono kwa asilimia mia moja sina tatizo nayo. Ahsante sana. (*Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru *Allah Subhana Wataala* aliyetujaalia kuweza kusimama hapa leo tukaweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha za Serikali, kama ulivyowasilishwa kwenye Baraza lako.

Pia napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe kunipa nafasi, lakini pongezi za pekee na sifa nyingi ziwaendee Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu na Kamati ya kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi nzuri waliyoifanya wakaweza kuwasilisha Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti mimi leo sitaficha hisia zangu, hisia zangu leo ziko wazi. Katika Miswada yote iliyowasilishwa katika Baraza hili hakuna Mswada umenifurahisha kama Mswada huu, hili natamka wazi hakuna kabisa Mswada uliokuwa ni mzuri nimeupenda kama Mswada huu, Mwanasheria Mkuu na Waziri hongereni sana, kwa sababu mnanirudisha nyuma wakati nilipokuwa nikichangia kwenye Hotuba ya Bajeti, nilimuomba mimi Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuweka mazingira mazuri ya Sheria zionazofuatana ambazo zinafanya kazi sambamba kwa taasisi zetu za Serikali, nilipoanza kuusoma mswada huu nikasema pale ninapotaka mimi tayari Serikali imeshapaona, sijui mumesikia kilio changu, sijui Mwanasheria ulinisikia siku ile ndio maana ukauleta huu au vipi, ahsante sana.

Kwa hivyo kabla ya kuchangia kwanza natamka, mwisho nitatamka tena, lakini natamka kwamba naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja, mimi napenda tena kusema kwamba Mswada huu umepangika, tena umepangika vizuri sana. Mfano nazungumza ukienda kwenye kifungu cha 3 (2) napenda kukinukuu.

"(2) Inapotokezea mgongano baina ya masharti ya Sheria hii na sheria nyengine inayotumika kusimamia jambo lolote linalohusiana na masuala ya fedha za Taasisi za Umma, masharti ya Sheria hii yatatumika".

Hii imeshaondoa mzizi wa fitna, hii inaipa nguvu sheria moja kwamba sheria hii itatumika na ndio vizuri nitoe wito tena Mwanasheria Mkuu kwa kuzipitia zile Sheria ambazo zote zina mapungufu uziweke namna hii, ili kurahisisha utendaji kazi wa Wizara mbali mbali za Serikali, tukienda kidogo jambo jengine ambalo ndio msingi na ambalo nimeuona mimi ni kwenye msingi wa usimamizi wa fedha 132 wa fedha za Serikali.

Lakini mimi hapa nataka nimuombe Waziri atakapokuja katika majumuisho aniambie jinsi ya udhibiti wa deni la Serikali, kwamba vigezo gani, maana yake katika majumuisho yake aniambie, ni mikakati gani watakayoichukua kwa wale watu ambao ni wakandarasi walishindwa kutimiza vigezo, wakashindwa kukamilisha zile kazi za Serikali na baadae kuisababishia hasara Serikali wanapoweka mikataba yao na Serikali wakashindwa kukamilisha zile kazi. Na kwa wale watu ambao wamekopa pesa za Serikali kwenye taasisi mbali mbali za fedha wakashindwa kurejesha.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka kutoa mfano kitu kimoja ambacho kinaniuma sana na kinanisikitisha, lakini naamini Mswada huu kwa nilivyousoma ndio dawa yao ndio muarubaini wake.

Mheshimiwa ukitembelea pale Kisauni kwenye Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi utakuta kuna vifaa vingi ambavyo vilikuwa vya mkandarasi, vimewekwa pale sasa hivi, zile tunaamini ni fedha za umma ambazo zinateketea pale mkandarasi kashindwa kumaliza kazi, zile pesa na vifaa vinashuka thamani siku hadi siku hakuna njia ya kuvitumia vimewekwa vimekaa kama dampu pale, hili Mhe. Waziri nakuomba mulitafutie ufumbuzi.

Lakini si hivyo tu, mimi nilikwenda Kibele Kwareni kule nilipokwenda Kwareni kutembelea nikaona kuna mapipa mengi ya lami, lami ambayo naamini inaweza pengine kujenga hata kilomita tatu, nne au hata kilomita tano za barabara, ni fedha za umma zinapotea lami ile ipo, mapipa yale yameanza kuoza, lakini si kwamba Serikali itapata hasara tu basi na uchafuzi wa mazingira hali kama hii Mheshimiwa iko haja ya Serikali kuitafutia dawa, na dawa yake ni sheria hii itakapoanza kutumika, naiomba Serikali baada ya kupitisha Mswada huu leo ifanye haraka, hatuwezi kumwambia Rais kwamba tufanyie kesho, maamuzi ni yake, lakini na sisi tunaomba kwamba baada ya kupitishwa tu hapa leo nitamuomba Rais aiharakishe kuipitisha ili iweze kufanya kazi kwa haraka kuzinusuru fedha za umma ambazo zina mwelekeo wa kupotea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sitaki kuchangia mengi kwa sababu jambo likiwa zuri ukiliongezea mambo mengi unaliharibu ile ladha ambayo imo, unaharibu utamu wa kile kitu kilichokusudiwa, kwa sababu sisi tutatia yetu pengine yatakuwa yanachusha chusha kidogo, kwa sababu sisi wengine si wataalamu wa sheria. Lakini kwa ufupi ni kwamba Sheria hii Mswada ulioletwa hapa mbele yetu ni mzuri ingawa una baadhi ya mapungufu ambayo naomba tuyarekebishe kidogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuna marekebisho kidogo twende kwenye *page* ya 131 mstari wa nne kutoka juu kuna marekebisho, 132 kuna lile neno fungu la bajeti hebu tuitizameni naona kidogo ilikuwa iwekwe vizuri kwa sababu pale inasomeka kwamba fungu la bajeti maana yake ni Taasisi inayohusiana na bajeti, mimi naona fungu la bajeti kuita taasisi hata tukienda kwenye tafsiri naona fungu la bajeti maana yake ni bajeti ya Taasisi inayohusika, sijui ni sahihi. Lakini hapa inasema fungu la bajeti maana yake ni taasisi, naomba tuiangalie kidogo tuifanyie marekebisho na masawazisho ikiwa inawezekana.

Msingi kwa usimamizi wa fedha ulioko kwenye namba tano kifungu kidogo cha 1(a) kudhibiti deni la Serikali kwa vigezo endelevu, mimi nilitaka nijue hivyo vigezo ambavyo tutavitumia vitakavyokuwa endelevu ukija uje utwambie kwa maslahi yetu, ili na sisi tupate kujua vizuri kwamba tumepitisha Mswada huu sasa umekuwa sheria, kwa hivyo vigezo vyetu tutakavyovitumia kudhibiti hizi pesa, vigezo endelevu ni moja, mbili, tatu.

Halafu kifungu chengine ni kifungu cha 5(e) kusimamia madeni na mali ya umma kwa namna ambayo haitakuwa mzigo kwa vizazi vijavyo.

Mimi nafikiri huu ndio msingi mkubwa wa Mswada huu, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, bila ya kuwa na utaratibu mzuri wa udhibiti na usimamizi wa madeni, tunaona madeni ya umma yanaongezeka, vizazi vyetu vitakuja kutulaumu na tutakuwa hatukuwatendea haki tukaja tukawaachia mizigo ambayo haijulikani kwa wakati huo kama wataimudu kuitatua au vipi. Lakini ili tuweze kuweka mazingira mazuri na tuweze kwenda vizuri na vizazi vyetu vinavyokuja tukawarithisha nchi vizuri, ni vizuri kuwa na udhibiti wa kusimamia madeni, ili tusije tukawaachia vizazi vyetu madeni.

Kifungu hicho hicho cha 5(g) kusimamia kwa umakini vihatarishi vya fedha. Hivi vihatarishi vya fedha ndio kitu kikubwa cha kukisimamia, tusitoe mwanya. Naamini kwamba ndani ya Mswada huu unapogeuka kuwa sheria tukishaupitisha na ukawa sheria umefunga kila kitu, hakutakuwa na njia ya kuacha kihatarishi chochote cha kuwapata wabadhirifu kuweza kutumia mianya ya kuweza kuleta ubadhirifu kwa fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheria mimi sijawahi kuona Mswada uliopangika na kama utatuletea yote kama hii mimi nitakuwa napiga kampeni kila siku ya kupitisha. Tufanyie vizuri kama hivi, tuwekee wazi kama hivi, ili na sisi tuweze kuchangia kwa umakini. Unapoleta mengine yakawa kinyume nyume na sisi tunaona Mheshimiwa, na sisi unatuondoa kwenye *position*. Kwa hiyo kwa hili mimi Mheshimiwa nasema ahsante sana, uendelee na mpango

huo, uendelee na utaratibu huo na sisi tupo pamoja na nyinyi, na tunakuungeni mkono kwa dhati, hatutotoa ruhusa kwa mtu ambaye anayetaka kufanya mambo yaliyokuwa siyo, tuleteeni mambo mazuri kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya mimi leo sitaki kusema sana nimesema kidogo tu. Natamka kwamba naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia, ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi kuwa miongoni mwa wachangiaji wa Mswada huu wa Fedha. Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kutuletea Mswada ambao hatutopata kazi kubwa sana ya kufanya marekebisho kutokana na Mswada umekuja vizuri.

Pia niwashukuru Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, tumepitia tumeona mambo mazuri japokuwa ni sehemu na sisi ya wadau tumeweza kuchangia na leo sitochangia sana kwa sababu na mimi ni katika sehemu ya wadau, lakini yapo maeneo naomba niyakazie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende moja kwa moja katika sehemu ya Nane ya Uanzishwaji wa Mfuko wa dharura kifungu cha 54 (1), (2), (3), (4) na (5) ambayo kwa ufasaha kabisa imezungumzia madhumuni hasa ya kuanzishwa kwa mfuko huu wa dharura.

Niungane na wenzangu ambao wametangulia kuleta mapendekezo haya, lakini pia nimuombe Mhe. Waziri pamoja na uwepo mzuri wa vifungu hivi basi kuwepo na *justification* ya kuonekana yale baadhi ya maeneo ya dharura hata pale tutakapokuja kuandaa kanuni baada ya sheria hii basi yaainishwe yale maeneo ya dharura na sentensi ibakie na yatakayofanana na hayo ili kupisha sehemu ya udanganyifu kwa wafanyakazi wa utumishi watakaokuwa hawaitakii mema wizara hii, kuja kukitumia kifungu hichi vibaya. Kwa hivyo tunajua yapo matokeo ya dharura mengine yanakuwa magumu kuyatabiri, lakini yapo yanayoweza kuainishika na Kiswahili safi tuseme tu kwamba na yale ambayo yatafanana na haya. Kwa hivyo vifungu hivi mimi naviafiki bali nilikuwa naomba tu marekebisho kidogo kama tutakubaliana na Mhe. Waziri na watendaji wake basi tuone ipo haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke eneo hilo niende Sehemu ya Kumi ya Kukopa, Kukopesha na Usimamizi wa madeni. Hapa pia niunge mkono. Lakini katika

kifungu cha 58(2) naomba nikikariri kidogo kinasema "Mikopo ya nje itakopwa baada ya idhini ya kutoka Baraza la Wawakilishi" Nilikuwa naomba na hapa tuendeleze maneno kama tutakubaliana wenzangu kuwa isomeke: Kwa mikopo ya nje itakopwa baada ya idhini ya Baraza la Wawakilishi ambapo itazingatia kuwepo katika mpango mkuu wa serikali uliopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika Sura ya Tatu katika kifungu cha 22. Hapa pana taarifa ambazo zipo *attached* na kifungu namba (1), (2), (a),(b), na kuendelea. Mimi nataka niongelee zaidi taarifa ya hali ya kifedha.

Mara nyingi tunapokuwa tunakwenda katika sekta mbali mbali, tunakuta taarifa na mfumo mmoja ambao wanafunga taarifa zao za kuonesha uwezo wa kifedha, lakini zipo taasisi za serikali zinatumia mifumo tofauti na maelekezo ambayo yanaonesha ule uwezo wao wa kifedha, mfano Benki ya *PBZ*. Mfumo wanaotumia sio mfumo ambao wanatumia mashirika haya.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuunda Kanuni naomba Mhe. Waziri azingatie kuainisha mfumo utakaotumika na serikali ambapo Mdhibiti atapewa mifumo yote ile inayotumika ili kuepusha zile kasoro zinazojitokeza, kwa sababu unaweza kwenda na Kamati wakati unahoji anakwambia sisi mfumo uliofungwa hatutumii kabisa, sasa hujui kama kosa la Mdhibiti au pana kosa la uainishaji wa ile mifumo ya ufungaji wa kifedha unaoainisha. Kwa hivyo namuomba sana, ingawa sina tatizo juu ya kifungu hichi, lakini katika kuweka sawa kuainisha ile mifumo ambayo itatusaidia katika kufanya kazi zetu vizuri, basi katika kanuni ambazo watatunga basi kuainishwa kwa mifumo ambayo itatumika hata kama ile *statement* itazingatia pale ambapo patatokezea mfumo mpya basi Waziri atautangaza ili twende vizuri au twende pamoja katika mazingatio haya ya fedha.
Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 123 kwa taarifa hapo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hapa Mhe. Waziri nilikuwa naomba niseme tu kwa maelezo ya ujumla pia napo sina tatizo ya vifungu vyote hapa. Isipokuwa tatizo langu kwamba zipo sekta za umma ambazo wakati fulani zinafanya uajenti wa serikali, mfano *ZRB* na taasisi nyengine, lakini natolea mfano tu, unapokwenda hasa na Kamati hizi kama *PAC* utakuta taarifa ambazo kazipitia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na zinazokuja hapa Barazani zile za mapato na matumizi ya kawaida. Lakini mfumo hasa wao kama ni *agent* wa serikali wanakusanya mapato ambayo yatakwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali, uchunguzi ule wa moja

kwa moja wanafanyiwa na nani na kama wanafanyiwa na *CAG* kwa nini taarifa zao zile haziji Barazani zinakuja taarifa zao nusu. Kwa sababu wao ukiwauliza *source* zao ni ngapi, watakwambia aah! labda tuna kianzio kimoja tulichokikodisha.

Kianzio cha pili ni asilimia tano tunayopata katika ule utaratibu tuliowekewa na serikali, kuwa tutakachokikusanya ndicho tutakachokipata. Kwa hivyo utakwenda kuiona asilimia tano, lakini ule mfumo mzima wa ukusanyaji wa pesa haukaguliwi. Sasa na hapa tunakuja katika kupitisha mapato na matumizi ya serikali hatuoni ile *performance* ya taasisi hii, ni kweli imetupeleka pahali pazuri au imetupeleka pahali pasipostahiki. Sasa hata ushauri na maelekezo ambayo yatakuwa yana mazingatio hayapatikani. Sasa namuomba Mhe. Waziri katika eneo hili nimezungumza mfano tu wa taasisi hiyo, lakini hata benki wao wanawekeza. Lakini utakwenda kukagua yale mapato na matumizi kwa msururu wa kawaida lakini zile *investment* zao wanazoandaa kama *treasury bill* watapata kiasi, ili ifike pahali serikali iwe na uwezo au Baraza hili liwe na uwezo wa kushauri nini kifanyike katika maeneo muhimu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hichi sina tatizo, isipokuwa kuna tatizo na kuonekana kuna maeneo tunapokwenda kufanya *auditing* hatuyafikii, sasa Mhe. Waziri utakapokuja kwa ujumla unijibu nini mkakati wa serikali katika kutusaidia katika eneo hili.

Mwisho kabisa naomba niende katika Sehemu ya Kumi na Tano ya Masharti ya Jumla kifungu 130. Nimekisoma hichi kifungu vizuri na kwangu mimi nilivyofahamu dhima yake ule wakati wa kufuta yale madeni lakini naomba tu Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kwa ufasaha kuonekana dhima hii kabla ya kuleta hapa taarifa zake za awali tutazipata vipi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi nishirikiane na wenzangu kuunga mkono Mswada huu kwa asilimia 98, mbili naweka za buti baada ya Mhe. Waziri kunijibu.

Baada ya hapo naomba niwapongeze sana kwa mara nyengine viongozi wote wa Wizara hii kwa kuleta kitu kizuri ambacho kitatusaidia katika nchi yetu ya Zanzibar. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji katika Mswada huu wa usimamizi wa fedha za serikali na Mashirika ya Umma. Kabla ya michango yangu kwanza nitoe shukurani za dhati kwa Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote,

hususan Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika kwa kuweza kuwasilisha Mswada huu muhimu ambao unafuta ile sheria iliyotungwa mwaka 2005.

Vile vile nichukue fursa hii kuweza kuipongeza Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa hotuba yao ya marekebisho yahusianayo na Mswada huu na hususan nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Yussuf, Mwakilishi makini wa jimbo la Fuoni kwa uwasilishaji wake, kwa kazi ngumu ambayo alikabiliana nayo hadi Mswada huu ukafika leo katika kikao hichi.

Vile vile niwapongeze Wajumbe wenzangu ambao wamenitangulia kwa michango yao mizuri yenye nia ya kujenga na kuimarisha suala zima la usimamizi wa fedha za serikali na mashirika ya umma katika serikali yetu.

Nichukue fursa hii kwa pongezi za pekee, nimpongeze Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuyachagua majembe, Waziri wa Fedha na Mipango na Mwanasheria Mkuu kwa kuweza kusimamia vizuri Mswada huu na kwa utendaji makini.

Nimpongeze sana Waziri wa Fedha kwa kuongeza mapato katika kipindi hichi kifupi na kuona uchumi wa nchi hii unapanda.

Baada ya pongezi na shukurani hizo, Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu mimi nimeupitia kifungu hadi kifungu na nimeupitia neno hadi neno.

Mswada huu wenye sehemu Kumi na Tano na vifungu 134 wa Usimamizi wa Fedha za Umma ni Mswada mmoja ambao naweza nikasema ni Mswada Bora kwa maana ya uzuri kutokana na kupangika kwake, lakini hata lugha fasaha iliyotumika.

Pamoja na hayo ni kwamba Mswada huu umesheheni maeneo mengi muhimu ambayo wakati mwengine yalikuwa yana kasoro ukilinganisha na sheria iliyopita, na kutokana na kasoro hiyo ilikuwa inasababisha mianya ya mapato katika ukusanyaji mzima au usimamizi mzima wa fedha za Umma. Vile vile umezingatia viwango kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Fedha kwamba utafiti umefanyika mpaka kutokea kwa marekebisho haya kuweza kuona kwamba sheria zetu za usimamizi wa fedha zinaendana na sheria za usimamizi wa fedha katika nchi mbali mbali ambazo zina usimamizi mzuri.

Nina imani kwamba Mswada huu utatusaidia sana katika suala zima la usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika hivi sasa nchi yetu ina wataalamu wengi wenye elimu za juu, wenye uzoefu mkubwa katika masuala yanayohusiana na usimamizi wa fedha. Nina imani kwamba wakielimishwa vizuri kuhusiana na Mswada basi ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa fedha utakuwa mzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa na wataalamu wazuri wenye elimu za juu na sheria nzuri hii ambayo tunatarajia tuipitishe, nina imani kwamba itapita, tuna changamoto mbali mbali zinajitokeza katika utekelezaji wa sheria zetu za usimamizi wa fedha.

Napenda nibainishe baadhi ya maeneo ili kusaidiana na Mhe. Waziri pamoja na watendaji wa sekta hii ya fedha.

i. Kasoro moja ni usimamizi hafifu wa sheria zetu.

ii. Ni kuwepo kwa kulindana na kufumbiana macho kwa watendaji wanaofanya makosa ya usimamizi wa fedha.

iii. Kuwepo kwa ukosefu wa maadili katika kada ya fedha kwa baadhi ya watendaji.

iv. Uwajibikaji hafifu wa baadhi ya watendaji wetu katika suala zima la usimamizi wa fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kuna makosa mbali mbali yanayojitokeza katika kusimamia fedha za umma, Taasisi na Mashirika ya Serikali. Moja ya makosa hayo ni mishahara hewa, hili suala linatupunguzia sana mapato, maana yake hakuna usimamizi mzuri katika baadhi ya taasisi ndio maana inatokea kuwepo kwa watumishi hewa ambao wanaigharimu sana Serikali.

Ya pili kasoro ambayo inajitokeza ni malipo ya mara mbili (*double payment)* kwa baadhi ya watendaji. Kwa masuala ya fedha utakuta kwamba kuna malipo ya mara mbili, mtu anaweza akalipwa kwa njia ya *cash* lakini vile vile ukaja ukaona kalipwa kwa njia ya *cheque*, sasa haya ni matatizo.

La tatu, kuna mapungufu katika *payment vouchers* zetu za watendaji mbali mbali. Wakati mwengine unaweza ukakuta *payment voucher* imesainiwa na mtu mmoja lakini kuna maeneo pengine matatu au manne yaweza kusainiwa ili kujenga uhalali wa malipo hayo. Lakini kukosekana kwa viambatananisho

muhimu katika *payment vouchers* hizo kama vile risiti, tiketi zilizotumika ambazo zinaleta ushahidi kwamba malipo hayo yameweza kufanywa kihalali.

Jengine ni malipo ya safari zisizo tija ni eneo moja vile vile la kasoro ambayo inaipunguzia sana mapato Serikali yetu na hii inaonesha kwamba hakuna usimamizi mzuri katika baadhi ya taasisi kuhusiana na jambo hilo. Inakuwa hakuna tathmini kwamba safari hii ina tija gani na inawezekana baadhi ya viongozi hutafuta mialiko ya makusudi ili waweze kufanya safari almuradi tu waweze kupata maposho. Sasa hii itakuwa ni hatari, usimamizi wa fedha hapa utakuwa si mzuri na kuna watu baadhi ya viongozi pengine anakwenda Dar es Salaam tu anaweza akashurutisha alipwe kwa njia ya dola. Haya tunayagundua katika taasisi ambazo tunapita na namuomba Mhe. Waziri alifahamu hilo ambalo halina ulazima. Sasa hapa inaonesha kwamba kuna woga katika baadhi ya watendaji wanaohusiana na mambo ya fedha katika hizo taasisi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna suala la risiti bandia na hususan hii inajitokeza katika Serikali za Mitaa. Kuna wakusanyaji wengi wa mapato wanapata mianya ya kuweza kutumia risiti bandia, hili tumelishuhudia tulipotembelea katika baadhi ya taasisi na kama tunataka usimamizi mzuri sana wa fedha basi suala hili la risiti bandia ambazo wanazitumia baadhi ya watendaji wetu wasio waaminifu liweze kuwekewa mkazo ili kuweza kuinusuru Serikali katika mapato yake, ili wananchi wa nchi hii waweze kupata maendeleo mbali mbali katika sekta za kiuchumi na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee hasa humu ndani ya huu waraka wa mswada huu.

Baada ya kupitia kifungu kwa kifungu neno kwa neno. Nimeona baadhi ya mambo niyazungumze ambayo yanaweza yakasaidia katika kuweka mswada huu kuwa bora zaidi.

Nikija katika Sehemu ya Kwanza hili ni suala la ujumla ndani ya mswada, kuna maneno yangerekebishwa. Neno "maalum" ningependa lisomeke "maalumu", kuna maneno mengi maalum yamo ndani ya mswada napendekeza yasomeke "maalumu".

Lakini kuna neno kipao au vipao mbele, katika Kamusi yetu ya Kiswahili sanifu hakuna kipao lakini kuna vipau, aidha kipaumbele au vipaumbele. Kwa hivyo ningependa na hayo maneno yasomeke hivyo.

Lakini kuna neno manunuzi, jana tulipitisha mswada wa sheria ya ununuzi, kwa hivyo ndani ya mswada huu ambao una maudhui yanayolingana na ule neno manunuzi ninafikiri lingetazamwa kila lilipotajwa ili lisomeke ununuzi.

Vile vile nipendekeze katika hii sehemu ya kwanza iongezwe tafsiri ya neno jukwaa la bajeti na uchumi, hili neno limejitokeza na ni neno geni, kwa hivyo ningependa sana lingetolewa tafsiri katika sehemu hii ya kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 131 haraka haraka kuna neno fungu, hili neno fungu naona ukiangalia na ile sheria iliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza naona kama halijakaa vizuri, kwa hivyo ningependa wataalamu kidogo wa fedha walitizame ili likae vizuri zaidi kuliko lilivyo hivi sasa.

Ukurasa wa 132 kwenye neno hazina ya Serikali, kwenye ile *version* ya Kiingereza pale inasomeka kwamba ni *Treasury* peke yake na sio *Government Treasury*. Kwa hivyo ningependa hata hiyo ya Kiingereza iweze kwenda mnasaba na hii ya Kiswahili.

Nikienda ukurasa wa 134 neno salio la fedha inasomeka kwamba maana yake ni bakaa la fedha. Ningependa hiyo la iondoke lakini iwe bakaa ya fedha, ninafikiri itapendeza zaidi.

Ukurasa wa 135 katika Shirika la Umma hapo kifungu hicho kuna *statement D* hapo ambayo imemalizia umma ambayo naona hiyo ni ilikuwa iondoke kwa sababu *statement* imeanza na Bodi, Kamisheni, Kampuni, Taasisi zinazoanzishwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria, Mfuko au Taasisi nyengine zisizokuwa mashirika ya umma ambayo hiyo ni iondoke ninafikiri haina mantiki itakuwa imeingia kwa makosa, halafu *statement* zinaweza kuendelea. Lakini hicho kifungu cha pili hapo pangekuwa na neno yanazopewa kuliko neno zinazopewa. Kwa sababu limemaliza mashirika, kwa hivyo mashirika isomeke yanayopewa na sio zinazopewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 137 hapa katika kifungu cha 7, kazi na uwezo wa Baraza la Mapinduzi hapa inazungumzia kazi za waziri.

Nilipousoma mswada ambao ulifanyiwa marekebisho kabla ya huu katika eneo hili kulikuwa na kipengele kimoja kizuri sana. Lakini katika mswada huu sikioni ambacho kilikuwa kinasema kwamba:-

Waziri husika wa Taasisi ya Umma atahitajika kuwasilisha katika Baraza Baraza la Wawakilishi:-

a) Taarifa ya Utekelezaji ya mwaka na taarifa za fedha zilizotajwa inaendelea.
b) Ilikuwa inaendelea mpaka kipengele cha 7 ambacho hakimo humu ilikuwa inasema:

   Ikiwa Waziri husika atashindwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji, taarifa za kifedha za mwaka za Taasisi inayohusika na bajeti ya Serikali au Taasisi ya Umma katika Baraza la Wawakilishi na Taarifa ya Ukaguzi wa Taasisi hizo ndani ya miezi 7 baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha Waziri husika atawasilisha kwa maandishi sababu za kushindwa kuwasilisha taarifa hizo.

Hii ilikuwemo lakini katika marekebisho haya ambayo yamefanywa na Kamati hiki kitu hakipo, nahisi ni kitu kimoja muhimu sana na katika kikao ambacho kilipita hapa hoja hii iliwahi kuzushwa na Mhe. Dimwa juu ya uwasilishaji wa taarifa.

Mimi napendekeza kama hakitoathiri basi kuna ulazima kwamba mawaziri wawasilishe ripoti zao za utekelezaji na utumiaji wa fedha kwa Baraza la Wawakilishi ili na sisi tuweze kujua na kujiridhisha juu ya utumikaji wa fedha ambazo tunazipitisha katika kikao hiki.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 138 kifungu cha 9 ambacho kinazungumzia Hazina ya Serikali kwa niaba ya Waziri. Kidogo hapa Mhe. Waziri atakapokuja aniwekee wazi kwa sababu kinasema hiki kifungu, Hazina ya Serikali kwa niaba ya Waziri itatekeleza kuna vifungu (a) mpaka (e) lakini hili neno kwa niaba ya Waziri ndio kidogo linanipa wasiwasi, kwa sababu Waziri mwenyewe yumo ndani ya Hazina hii sasa kidogo hapa inanipa wasiwasi, ningependa Waziri aje aniwekee wazi kwa nini ikaingia hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kifungu cha 10 kuna *statement* ya kwanza hapo ya (a) itahakikisha pawe na neno kwamba napendekeza, itahakikisha kwamba uandaaji, utekelezaji, usimamizi na uratibu wa sera za fedha ili hii iondoke kwamba hii ije pale juu ninafikiri ndio inaweza ikasomeka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kabla hujanichoka nije ukurasa wa 142, lakini kama nitakuwa muda wangu unafifia kwa leo ningependa kidogo muda wa nyongeza.

Ukurasa wa 142 kifungu cha 17, uwezo na majukumu ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Hapa twende katika kifungu cha (d) kinasomeka kuajiri, kutoa

mafunzo na inaendelea, wasiwasi wangu uko katika suala la kuajiri. Suala la kuajiri ambalo amepewa huyu Mhasibu Mkuu.
Naelewa kwamba Serikali ina Sheria ya Utumishi, kuna Tume ya Utumishi ya Serikali, sasa sijui kuna mantiki gani hapa kwamba Mhasibu Mkuu amepewa jukumu la kuajiri wakati Sheria ya Utumishi ipo na Tume ya Utumishi ipo. Ningependa Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutuwekea bayana maudhui au mantiki ya kupewa mamlaka ya kuajiri kiongozi huyu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 146 katika kifungu cha 25 namba 2 kuna *statement* inayosema Hazina ya Serikali itatunga Kanuni za kuwaongoza, kuwaongoza kwa maana ya kwamba hapa tulitarajia kuwe na watendaji wengi, lakini iliyojitokeza ni mtendaji mmoja, Afisa Mhasibu. Kwa hivyo kama ni peke yake aliyepo hapo basi iwe ni kumuongoza na sio kuwaongoza.

Lakini tukija katika ukurasa wa 147 kifungu cha 27 mstari wa 5 neno viashiria hatarishi iwe vya kifedha na sio za. Lakini vile vile tukija katika kifungu cha 2(d) ambacho kinasema mfumo wa kutathmini miradi yote ya mikubwa, hiyo ya nafikii hapo ilikosewa itoke iwe inasomeka miradi yote mikubwa.

Kifungu cha 28(2) kuna neno limeanzia na maafisa lakini tukiangalia *statement* ya juu, tukija hapo hapo kwamba Mhasibu, sasa sijui kama ilikuwa ni maafisa wahasibu au Afisa Mhasibu. Kwa hivyo ninafikiri lingeweza kutazamwa vizuri hilo neno likaenda na muktadha ambao umekusudiwa.

Ukurasa wa 148 kifungu cha 30(2), kutokana na *statement* ya namba 1 huyo muhusika alikuwa awe Afisa Mhasibu na sio Afisa mas-ul. Kwa hivyo turekebishe hapo isomeke hivyo kwamba ni Afisa Mhasibu.
Tukija ukurasa wa 179 Mhe. Mwenyekiti, kifungu 105 chombo cha usimamizi. Katika kifungu hiki imesomeka hapo mwanzo kwamba chombo cha usimamizi kitahakikisha kuwa Shirika la Umma halafu ikaendelea. Lakini kuna neno kifungu cha 1 kimesema, viashiria lisomeke kwamba ni viashiria.

Kifungu cha 3 kuna neno manunuzi ambayo ningependa iwe ununuzi lakini tukija kifungu cha (b), kifungu cha (b) kimetajwa litachukua hatua muafaka za ufanisi. Sasa huku kimetajwa chombo cha usimamizi kwa hivyo ikawa ni li, lakini iwe ni ki, kitachukua na hiyo ki iendelee katika vifungu vyengine vyote vinavyofuata chini hadi kifungu cha h isomeke ki kama ni chombo basi isomeke ki isiwe vyenginevyo.

Vile vile kutoka kifungu (b) kikafuata na kifungu (b) chengine kwa hivyo vifungu (b) utavikuta ni viwili. Kwa hivyo kutoka ile (b) nyengine iendelee kuwa ni (c) kwa hivyo isomeke c, d, e na kuendelea uwe na mpangilio mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa muda ambao umenipa na mimi nishukuru vile vile kwa michango ambayo nimeitoa, na nina imani kwamba michango hii inaweza ikamsaidia sana Mhe. Waziri katika kuweka sawa mswada huu, lakini nisisitize tu kwamba mswada ni mzuri lakini uzuri huu bila ya kuwa na watendaji waadilifu, bila ya kuwa na usimamizi mzuri wa sheria hii basi itakuwa ni ndoto.

Mategemeo yetu kwamba Serikali yetu hii iweze kukusanya mapato kwa kiwango kikubwa, ili miradi mingi ya maendeleo iliyopo katika majimbo yetu iweze kukwamuka na wananchi waweze kupata faraja ya Serikali hii.

Baada ya kusema hayo machache, nikushukuru sana. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima tena naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa wasaa wa kuweza kupata afya, na kuweza kutimiza hayo ambayo ni majukumu ambayo tumepewa na taifa.

Kwanza pia na mimi niwashukuru sana vyombo vyote vinavyoandaa miswada kwa pamoja kuhakikisha kwamba miswada inatufikia hapa na kupata ridhaa ya Baraza ili kuweza kuendelea ili itumike vizuri.

Mwanasheria Mkuu, Waziri, Katibu Mkuu Kiongozi pamoja na watendaji wengine wote. Wizara ilianza kufanya uhakiki wa pensheni kuna nani wanastahiki na wapi wameingizwa kimakosa.
Mhe. Rais alipata ulalamishi wa kutotekelezwa vizuri huduma hii ambayo imetupa sana heshima ya nchi yetu na pia umetoa huduma na kuwapa watu wetu moyo wa kuona kwamba wana haki katika michango hiyo waliyoifanya katika nchi hii katika maisha ya wote.

Kwa kawaida Wizara ya Fedha ina utaratibu uliokuwa unatumika katika utekelezaji wake wa shughuli zake za kawaida za siku zote na usimamizi wa fedha chini ya Mhasibu Mkuu na taratibu nyengine.

Mimi nimefarijika sana kuona katika sehemu ya 13 ya taarifa ya mwaka ya ukaguzi wa waangalizi kifungu namba 14 ambacho kinasema kuwa:

“Kuanzishwa Idara ya Ukaguzi wa Ndani chini ya Wizara inayoshughulikia fedha itakayojulikana kama Idara ya Ukaguzi wa ndani ambayo itaongozwa na Mkaguzi Mkuu wa Huduma za Ukaguzi wa Ndani”.

Kitu ambacho naamini kabisa kwamba wakishakuwa na Idara yao Utendaji utakuwa ni mwepesi zaidi kuliko kungoja kupata taarifa au maelekezo mengine katika sehemu nyengine. Kutayarishwa kwa Sera za Ukaguzi wa ndani na kununua au viwango miongozo na maelekezo, jambo ambalo utaratibu mzuri utakuwepo katika kutekeleza yale yote ambayo wananchi wanayatarajia na kunufaika nayo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niseme tu kwamba suala hili linatupa faraja kuona kwamba fedha zetu za Serikali hazitatumika vibaya, na pia kwa jinsi hii napenda nitoe tu shukurani na pongezi za pekee kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa upendo na umakini kwa suala hili la huduma ya jamii ikiwa ni pamoja na pensheni.

Siku ya sherehe siku ya wazee alituzindulia kuangalia utekelezaji wa huduma hii kwa makini. Sisi wenyewe tulipokuwa tunatekeleza tulijua kabisa ule uandikishaji kwa kupitia masheha, kwa kupitia ma-*DC*, ndugu na marafiki wanaofahamika ulikuwa unafanyika vizuri. Lakini akaja kugundua kwamba kuna masuala machache machache yaliyokuwa na udanganyifu ambao haukupendeza.

Mhe. Mwenyekiti, kusema wazi kuwa hatamezea wala kupuuzia watendaji wasio waaminifu katika kutekeleza majukumu yao. Hivyo basi, niungane na wale wote ambao wanaunga mkono jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nitoe wito kabisa kwa wazee wetu wanaolipwa na wanaowezeshwa sasa hivi kwa mara ya kwanza, na wale ambao tayari wako katika orodha hawajalipwa kwa sababu zoezi hili linaendelea na waliokwisha kujiandikisha wote watalipwa bila ya hofu. Kukawia kuwafikia ni kazi mojawapo ya kuhakiki ili kila mtu apate haki yake.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamaliza napenda niseme tu kuwa naunga mkono mswada huu na kuungana na wale wote waliounga mkono mswada huu kwa usimamizi wa fedha za umma na mkaguzi kwenye kipengele Nam. 114(2) anasema mkaguzi baada ya uanzishwaji wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani urasimu utapungua na matokeo ya usimamizi yatakuwa mepesi.

Baada ya haya nipende kuunga mkono asilimia mia moja kwamba uanzishwaji wa mswada huu utakuwa ni faraja kwa wengi na hasa kupunguza mlolongo wa ufuatiliaji unapokuwa na urasimu mwingi pasipokufikia mambo ya maamuzi au utekelezaji kwa wakati mfupi. Naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuchangia huu mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma na Mambo Yanayohusiana nayo.

Kwanza na mimi nachukua fursa hii kuwapongeza taasisi zote ambazo zilishiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha kazi hii adhimu kabisa yenye manufaa kwa wananchi wetu.

Hapo mwanzo nilikuwa najiuliza kwamba ipi ingekuja mwanzo, sheria ya usimamizi wa fedha au sheria ya usimamizi wa mapato. Lakini hata hivyo, nikaona yana uzito sawa, sasa nianze kwa kuangalia baadhi ya vifungu lakini kabla ya hapo niseme kwamba kwa tafsiri yangu naona kwamba sheria hii imekuja kwa ajili ya kuweka nidhamu bora zaidi za usimamizi juu ya matumizi ya fedha za umma. Kama hivyo ndivyo, basi ningeishauri wizara kusimamia sana suala la nidhamu katika vipengele vyake mbali mbali hasa wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Kwanza nidhamu ya utendaji lazima wafanyakazi wanaosimamia mfumo huu wa matumizi ya fedha, lazima wajengeke katika kufanya kazi kwa kuzingatia weledi wao, utaalamu wao, kwa kuzingatia kanuni zinazoongoza masuala ya fedha, sheria zinazosimamia fedha lakini pia kama kuna miongozo inayosimamia fedha. Mambo haya ni muhimu sana. Inawezekana kinachokosekana kwa sasa kwa baadhi ya watendaji hawa ni nidhamu hii ya usimamizi wa masuala haya.

Jengine muhimu la kuzingatia Mhe. Mwenyekiti, ni suala la uweledi katika kazi hii ya uhasibu. Nadhani wakati umefika kwamba kazi hizi kufanywa kwa weledi mkubwa kabisa badala ya kufanya kazi hizi za uhasibu kwa mazoea. Weledi lazima upate nafasi yake na lazima ufuatiliaji uwe makini sana ili kuona kwamba wanaofanya kazi wanafanya kazi kwa weledi badala ya mazoea.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine mimi naita nidhamu ya wakati nalo ni muhimu sana katika kufanya kazi hizi za uhasibu. Jambo ambalo linawezekana kufanywa kwa nusu saa lifanywe kwa nusu saa, jambo linalowezekana kufanywa kwa wiki basi lifanywe kwa wiki wala isiwe miezi miwili au mitatu.

Jambo hili nalo lazima tulisimamie ikiwa tunataka tufanikiwe katika kudhibiti matumizi ya fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine muhimu kabisa ni nidhamu ya uongozi na hapa ni suala zima la usimamizi, lazima tufanye kazi, lazima viongozi wasimamie majukumu yao ili kuona kwamba masuala ya matumizi ya fedha yanakwenda kama zinavyotakiwa na miongozo, sheria na kanuni iliyopo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine nalo nilikuwa naangalia watu muhimu kabisa waliotajwa katika sheria hii ikiwa ni pamoja na Waziri, Katibu Mkuu, Mlipaji Mkuu, Mhasibu Mkuu na wengineo, na bahati nzuri wamefafanuliwa vizuri pamoja na kazi zao. Ni sawa, lakini mimi nilishauri kwamba ni vyema baadae ili kuondoa mgongano katika utendaji wa kazi zao ningeshauri kwamba katika wakati wa kuandaa kanuni za fedha suala hili lipewe nafasi ili kuweka mipaka, Katibu Mkuu mpaka wake ni upi, Mhasibu Mkuu mpaka wake ni upi. Jambo zuri zaidi likapata ufafanuzi katika kanuni kuliko kubakia hivi hivi katika sheria huenda likaleta mkanganyiko hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa makusudi kwa sababu sheria hii katika baadhi ya vifungu inamuelekeza waziri kutengeneza kanuni, lakini baadhi ya vifungu imekaa kimya. Sasa mimi ningependa kumzindua tu waziri kwamba baadae waipitie kwa makini hata zile sehemu ambazo labda sheria haikusema ikionekana kuna haja ya kufanya hivyo waziri afanye hivyo kwa ajili tu ya kurahisisha utekelezaji na ufanisi katika kazi hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningependa kushauri nalo ni hiki kifungu cha 26(4) cha sheria hii. Hiki kimesema kwamba ningependa ninukuu.

"Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha kifungu hiki, Mlipaji Mkuu wa Serikali anaweza, katika mazingira maalumu kumuagiza kwa maandishi mtu ambaye sio Mtendaji Mkuu wa Shirika la Umma au Serikali ya Mtaa kuwa Afisa Mhasibu".

Hapa na mimi ningeshauri iwepo kanuni ambayo itamuelekeza Mhe. Waziri kumteua mtu wa aina gani. Katika uwazi huu anaweza akateuliwa mtu yeyote hata tarishi akateuliwa na waziri. Kwa hivyo, nadhani kanuni isaidie kuwabainisha baadhi ya watu ambao wana sifa ya kuweza kuteuliwa kufanya kazi kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na suala hilo kuna suala hili ambalo limezungumzwa vizuri linalohusiana na fedha na bajeti. Suala hili nalo linafaa

kutizamwa kwa makini sana, kwamba tuandae bajeti kwa mujibu wa fedha zilizopo na hii itatusaidia hata katika udhibiti. Kwa hivyo, napenda sana kushauri kwamba wakati wa kuandaa bajeti basi tuzingatie sana uwezo wa kifedha uliopo, na hiyo itatusaidia kujenga bajeti halisi au bajeti yenye uhalisi, na hili ni muhimu na sheria imetaja suala hilo. Lakini ningeshauri tu wakati wa utekelezaji tuzingatie masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nilikuwa nataka kulisema ni suala sikuliona sijui labda ningetaka ufafanuzi baadae, unapotizama katika muundo wa Wizara ya Fedha ya Muungano katika sehemu ya Hazina kuna mtu anaitwa Msajili wa Hazina. Hapa katika sheria yetu sijaona mtu huyo na ni muhimu sana, labda inawezekana anafanana na mlipaji mkuu au na mtu mwengine yeyote nataka ufafanuzi baadae kuhusu suala hili la Msajili wa Hazina.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kulisisitiza sana na hasa katika hatua ya utekelezaji baadae. Nadhani wakati umefika kwa Wizara ya Fedha kuandaa kwa makusudi maadili ya kazi za uhasibu badala ya kufanya kazi kwa kanuni za ujumla za maadili, ambazo pengine mhasibu amesoma chuoni, mhasibu anatakiwa aende hivi na hivi na hivi. Nadhani sasa wakati umefika kwamba wizara hasa kuandaa *Professional Codes of Conduct* ya uhasibu ambao wahasibu wote watalazimika sasa kuifuata, ambayo bila shaka itakuwa na mambo gani mhasibu anapaswa kufanya, yapi hapaswi kufanya na mengineyo yanayohusiana na *profession* hiyo. Na hii ni njia moja ya kuithamini kazi hii ya uhasibu, lazima tuithamini na njia moja ya kuithamini ni kuiundia kanuni ambayo mhasibu atakuwa kwa kweli analazimika kuifata. Lakini kwa utaratibu huu wa jumla ambao tunakwenda nao sasa itakuwa ni vigumu wakati mwengine kuwasimamia ipasavyo watu wanaofanya kazi hizi za uhasibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia niseme kwamba naunga mkono mswada huu, na kwa kweli nawaomba Wawakilishi tuunge mkono mswada huu ili utusaidie katika kudhibiti matumizi ya fedha, lakini wakati huo huo namuomba tena Mhe. Waziri afikirie pia kufanya utafiti juu ya sheria hii inayosimamia masuala ya mapato nayo pia ina mapungufu basi itayarishwe na iletwe Barazani kwa ajili ya kujenga mafanikio zaidi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nataka kutoa shukurani za dhati kwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akisaidiwa na Katibu Mkuu wake wa wizara hii, kwa kweli watu hawa wawili wanafanya kazi nzuri kwa serikali yetu na wanajitolea na kazi kubwa kabisa.

Nataka kusema Mhe. Mwenyekiti, kwamba wizara hii ndio *engine* ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuleta maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, uzuri wa mswada huu ni matunda ya utekelezaji wa sera za CCM, ambazo wakati tuko wagombea urais, lakini mgombea urais wa CCM Dkt. Ali Mohamed Shein alinadi sera zake. Kwa hivyo, nataka kusema kwamba wale vyama wenzetu ambao tulikuwa katika uchaguzi hii ni ishara tosha kwamba wenzetu wanatekeleza sera nzuri kwa ajili ya manufaa ya wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile sisi pia tuliokuwepo hapa kutoka vyama vya upinzani lakini kazi yetu kubwa ni kutekeleza sera za Chama cha Mapinduzi. Maana tulikula kiapo kwa kukamata *qur-an* tukufu mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Pia nataka kusema kwamba Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein alishaanza kuchukua hatua mbali mbali juu ya kubana matumizi kwa gharama za serikali. Lengo lake ni kutaka kuwapatia wananchi wa Zanzibar manufaa na maendeleo. Kwa bahati mbaya Rais wetu si mtu mwenye kupenda sifa sana kama watu wengine, lakini nataka kusema kwamba kuna hatua nyingi ameshachukua mbali mbali za kudhibiti matumizi ya serikali kwa kubana matumizi, mambo mengi amefanya lakini bahati mbaya si kiongozi ambaye anapenda sifa, kwamba kila alifanyalo atangaze kwenye vyombo vya habari.

Lakini katika kubana matumizi hayo fedha nyingi zipo ambazo sasa hivi tunaona maendeleo, na haya maendeleo yanayopatikana kwa mfano juzi tu hapa tumeona hospitali ya Mnazi Mmoja ikiwa na vifaa vya kisasa kwenye wodi ya mama na watoto. Sasa hii ni kubana matumizi na tumeona juzi hospitali ya Abdalla Mzee pamoja na kwamba kuna misaada lakini pia serikali ziko fedha zake, na tunashuhudia faida ya kubana matumizi kwa serikali yetu sasa hivi kuna miradi mingi ya maendeleo inakuja wakati wowote itazinduliwa kuelekea sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwaomba wale watendaji ambao wana dhamana za serikali sasa hivi tubadilike kama Mhe. Rais anavyosema tusifanye kazi kwa mazoea.

Mhe. Mwenyekiti, sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa hivi tuna kiwanda kikubwa na kizuri na cha kisasa na chenye vifaa ambavyo hata nchi za Afrika hawana, Kiwanda cha Uchapaji. Napenda sasa wataalamu wetu tukitumie kiwanda hiki kwa kupeleka kazi zetu, si mahala pengine kwa ajili ya

kubana matumizi, na kwa ajili ya kukifanya kile kiwanda chetu kipokee kazi mbali mbali. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba mimi nimesimama hapa kuwapongeza wale wote wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi kwa michango yao mizuri waliyotoa na michango yao ya kizalendo kwa mapenzi ya serikali yetu na taifa letu. Lililo mbele yetu sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuwaomba wakati wa kupitisha vifungu sote kwa pamoja tusimamie tupitishe vifungu hivi ili mswada huu uweze kupitishwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache mimi Juma Ali Khatib, Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi na ningependa tu niseme kwamba mswada huu ambao umewasilishwa leo naweza nikasema kwamba ni sawa na mlingoti wa bendera ama tunaweza tukasema mlingoti wa jahazi ambao unaweza ukavusha watu walio ndani ya chombo. Kwa sababu jahazi kama halina mlingoti basi safari yake inakuwa ndogo sana, na pahala kama hakuna bendera watu wanashindwa kuelewa umuhimu wa pahala hapa. Kwa hiyo, mswada huu umekuja kwa umuhimu mkubwa ambao utawawezesha Wazanzibari kupata maendeleo makubwa katika kipindi kifupi tu kijacho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu kazi kubwa ambayo imetukabili sote ni kusaidia kudhibiti matumizi mabaya ya serikali, kudhibiti upotevu wa fedha unaofanywa na watu wachache kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuna watu kwa makusudi hufanya sherehe za serikali kuwa *deal* la kupoteza fedha za umma. Fedha za umma zinapotea wananchi wa kawaida wanashereheka kwa maana ya sherehe, lakini baadhi ya watendaji wanashereheka kuwa ni *deal* la kupatia fedha. Sasa sisi kama viongozi tunahitaji kuhakikisha kwamba tunasaidia kwa nguvu zote serikali ili mapato yale yasipotee bure na wananchi waweze kufanyiwa zile huduma muhimu ambazo zinalazimika kufanywa, kama vile barabara, umeme, madawa na mambo mengi tu ambayo ni ya umuhimu kwa jamii.

Leo tumeshuhudia ni miaka 52 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendelea na mfumo wa elimu bure na walimu wanalipwa mishahara mizuri, mikubwa. Kwa nini? Ni kutokana na kwamba fedha inakusanywa wanapewa wao. Lakini ni vizuri sasa tukaendelea na udhibiti ili tukaweza kufika pahala pa kuweza kutoa changamoto zaidi ya yale mambo ambayo yamekwaza. Kwa vile

udhibiti wa fedha unatokana na watu waliosoma, watu ambao leo tunao wengi sana hapa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, tuna wahasibu wazuri tu ambao wamesoma Chwaka, wamesoma Tunguu na sasa wanasubiri ajira kwa ajili ya kwenda kufanya taaluma yao waliyonayo. Kwa sababu masuala ya fedha yanahitaji zaidi taaluma, taaluma ya kuidhibiti fedha, taaluma ya kuitumia fedha inavyotakiwa, taaluma ya kuipeleka fedha inapotakiwa kisheria ndio muhimu zaidi katika hoja nzima ya fedha. Sasa leo serikali kwa muda mrefu ilikuwa inapigiwa kelele kwamba fedha zinatumika vibaya, zinapotea vibaya, zinakwenda ovyo. Sasa hii ilitokana na wachache wanaotaka utajiri wa haraka na wakashindwa kuona kwamba mlingoti wa kutufikisha pazuri ni mapato yanayodhibitiwa.

Sasa sisi kama serikali tunatoa wito kwamba ni vyema matumizi yanayotumika katika Serikali za Wilaya, Serikali za Mkoa, Serikali za Jimbo yakatumika kwa umadhubuti zaidi, kwa uangalifu zaidi na kwa maana ya kwamba udhibiti pia uwe ni mkubwa zaidi.

Sasa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao ni sehemu ya kuchunga udhibiti wa fedha hiyo zisitumike vibaya. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni serikali, hapo ndio serikali ilipoanzia na ndio maana Chama cha Mapinduzi kikawa kinahangaika kufa na kupona kupata Wawakilishi wengi ili kiweze kuunda serikali. Kwa upande wa Rais huwa hawana matatizo, lakini wanahangaika kutafuta wawakilishi ili waunde serikali. Sasa wawakilishi ni sehemu ya serikali wana haki ya kuona matumizi mabaya yanakwenda vibaya na kwa haraka sana wakatoa taarifa kwamba hapa kinachochezewa ni pesa ya umma na hatuhitaji kuona pesa ya umma inachezewa. Wasisubiri mpaka jahazi lishatota ndio mtu anakaa pembeni anasema kwamba aah mimi nilimuona yule ana matumizi mabaya, anawalipa watu kwa dola, anaondoka anakwenda Dar es Salaam asubuhi jioni anarudi, nilimuona mimi ananunua gari hili na hili, ana majumba 50.

Sasa wewe kama mwakilishi wewe ni serikali toa taarifa kunakohusika tudhibiti hayo matumizi mabaya, kwa sababu hiyo fedha ni ya umma, walala hoi waliopo kila pahala nchi hii hiyo pesa ni yao na wewe unayejifanya unatumia, unatumia vibaya matumizi mabaya ya pesa ya umma. Kwa hiyo, sisi kama wawakilishi bado tuna dhamana ya kuisaidia serikali kwa namna moja au nyengine kuwafichua wale wote ambao wana matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu hii ni awamu ya aina yake, yenye uwezo mkubwa na yenye wawakilishi mahiri, kwa sababu walihangaika kuingia kwenye uchaguzi kwa nia ya kutaka kuongoza serikali. Kwa hiyo, hawako tayari, naamini hivyo Mhe. Mwenyekiti kwamba wawakilishi hawa hawako tayari kuona matumizi mabaya ya mtu anayaendeleza. Na sisi kama serikali tunawaambia hao walio na mwendo huo wa kutumia matumizi mabaya ya serikali waache mara moja, tukiwagundua wala hatutawavumilia, kwa sababu tunahitaji kufanya yale ambayo Rais ameyaagiza katika kugombea kwake, na hayatafanyika kwa maneno lazima yaambatane na vitendo, na vitendo bila ya pesa hakuna. Kwa hivyo, tuko tayari kusema mtu yeyote aliyekuwa hatokuwa na uwezo wa kuwa mdhibiti mzuri wa fedha za umma basi akae upande haraka sana kabla hatujamuondoa, sasa hatutavumilia matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hii na nawaomba wawakilishi tupitishe hoja hii kwa maana ni maslahi makubwa kwa Wazanzibari wote ili fedha yetu iwe inatumika kwa kwa maslahi ya nchi yetu.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said kwa mchango wako, lakini pia niwapongeze wachangiaji wote waliochangia kwa muda huu na pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa kuwasilisha vizuri.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kutuletea mswada huu.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha tuna dakika 15 lakini nitaahirisha ili waheshimiwa wapate nafasi ya kwenda kwenye msiba wa Mheshimiwa mwenzetu aliyefiliwa na mtoto wake. Pia mchangiaji ambaye aliyebakia kuchangia ni mmoja atakuja kuchangia kipindi cha jioni naye ni Mhe. Waziri wa Habari na Utamaduni.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaahirisha kikao hiki mpaka saa 11:00 jioni. Ahsante.

(Saa 6:43 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11: jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika ahsante sana.

Awali ya yote kwanza nichukue fursa hii kukupongeza wewe kabisa kwa kunipa nafasi hii adhimu; lakini pia nimshukuru Mola (*S.W*) kwa kuweza na mimi kunipa nafasi na pumzi ya kuweza kuchangia hoja yetu hii iliyo mbele yetu kuhusiana na usimamizi wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa wale wote waliotayarisha mswada huu, na hii leo hatimaye kukamilika na kuweza kuletwa mbele yetu ili kuweza kuuchangia, na bila ya wasiwasi wowote kuweza kuupitisha muda mfupi ujao.

Mhe. Naibu Spika, napenda sana nitoe pongezi zangu za pekee kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa umahiri aliouonesha katika kuweza kuusimamia na hatimaye kuamua kabisa kufuta sheria iliopo na kuleta mswada huu ambao utakuwa na sheria mpya kabisa. Naelewa wazi kwamba suala la fedha kwa kawaida hugawika katika sehemu kuu mbili, sehemu ya mapato na sehemu ya matumizi.

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kwamba Baraza lako tukufu limeweza kufanya kazi kubwa sana ya kutunga sheria mbali mbali zinazohusiana na usimamizi wa fedha katika ukusanyaji wa mapato.

Vile vile Baraza lako tukufu leo hii linaweza likakamilisha kazi kubwa zaidi ya kuweza kutunga sheria ya kusimamia matumizi ya fedha ambayo yanatokana na mapato yanayokusanywa na wananchi wa nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naelewa wazi kwamba mswada huu una umuhimu mkubwa sana, na ndiyo maana leo ukafikishwa hapa mbele yetu. Ni wazi kwamba mswada huu umefika kwa wakati muafaka, kwani malalamiko mengi yalikuwepo hapo nyuma juu ya matumizi ya fedha za umma, lakini naamini wazi kwamba kupitishwa kwa mswada huu basi itakuwa ni changamoto kubwa katika kuzisimamia vizuri fedha za umma.

Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma unaweka masharti bora ya kudhibiti na kusimamia fedha za umma pamoja na mambo mengine yanayohusiana nayo, una umuhimu mkubwa kwa kuweka umakini wa kusimamia fedha za umma ambazo wananchi huchangia kwa hiari kabisa kupitia kodi, ada na mapato mengineyo.

Mimi nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Amani nachukua fursa hii kuwawakilisha wananchi wangu kukubaliana kabisa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, katika kuuleta mswada huu hapa na kuuchangia, kuujadili na hatimaye kuweza kuupitisha. Naamini wananchi wangu ni wachangiaji na walipaji kodi bora. Hivyo, walikuwa na imani kubwa katika mapato yao yote yanayokusanywa kupitia serikali hii kuona kwamba yanatumiwa katika umakini mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Amani wana muamko mkubwa katika kusikiliza taarifa hususan zinapogusa matumizi ya fedha za serikali. Lakini kwa muono mkubwa na wao wanaunga mkono mimi kuwepo hapa kuweza kuuchangia ipasavyo, kukubaliana na vifungu vilivyokuwemo, kwa sababu imani yao ni kwamba itakapofika wakati wa kutumika sheria hii basi huduma zilizo bora kwa jamii zitafika bila ya upendeleo na zitafika bila ya dhulma za aina yoyote.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi sina mashaka yoyote na vifungu vilivyomo katika sheria hii inayotungwa hapa leo, ingawaje sheria ya zamani ilikuwa inalalamikiwa sana, lakini jitihada za wazi zilizofanywa na serikali kuona kwamba sasa umefika wakati kuziba yale mapengo yaliyokuwepo, udhaifu uliopo katika sheria hizo na kuweka vifungu vitakavyotoa ufafanuzi zaidi katika usimamizi bora wa sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, nafarajika sana kwa sehemu zote 15 zilizotungwa katika sheria hii, masharti yote yaliyomo ambayo yanaonesha usimamizi wa fedha yanaonesha wazi kwamba yamepangwa, yamewekwa na yamepitiwa vizuri kiasi kwamba yataondoa utata mwingi ambao hapo nyuma ulikuwa unaonekana. Nimevutika sana na sehemu tano kati ya sehemu zote zile zilizotungwa katika sheria hii, ingawaje sina wasi wasi wowote katika zile sehemu nyengine zilizobakia.

Napenda kupongeza katika ile Sehemu ya Pili, Uwezo wa Kazi za Baraza la Mapinduzi. Mswada huu umezingatia sana uwezo na kazi za Baraza la Mapinduzi kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya Pili, hii tukiipitisha Wajumbe wenzangu, tukiichangia vyema tunaweza kufikia pale pahali ambapo pataonesha umuhimu wa kazi za mihimili ilivyogawanyika.

Kuna masharti yaliyowekwa katika shughuli zote za Baraza la Wawakilishi, lakini sehemu ya pili imeainisha kazi maalumu zinazotakiwa kufanywa na Baraza la Mapinduzi.

Sehemu ya Tano Mheshimiwa imeonesha Masharti ya Dhamana za Wahasibu. Hii ni katika sehemu moja muhimu sana katika mswada huu. Ni wazi kwamba wahasibu wetu wamekuwa wakilalamikiwa sana, na serikali tayari imechukua jitihada za kuona ikiwa wahasibu walionekana kuwa ni chanzo cha migogoro na matatizo ya matumizi ya fedha za umma, kwa hivyo mswada huu leo umezingatia kwa dhati kabisa zile dhamana za wahasibu. Napenda sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wazitizame dhamana za wahasibu ili tunapokuja kuchangia yale mapungufu yanayopatikana katika matumizi ya fedha za umma basi zilalamikiwe kwa mapungufu ya sheria yatakavyojitokeza.

Nimejaribu sana kutizama Sehemu ya Sita ya mswada huu juu ya masharti ya uandaaji na udhibiti wa bajeti. Hiki ni kifungu ambacho Wajumbe wote humu kinawagusa. Moja katika kazi kubwa ya Baraza lako tukufu ni kupitisha bajeti za serikali baada ya kuzingatia kwa kina jinsi zilivyotayarishwa na jinsi zitakavyotumika.

Mhe. Naibu Spika, serikali imetumia nafasi hii kutizama mapungufu yaliyokuwepo, kutizama matatizo yaliyokuwepo na kutoa mwelekeo mpya kabisa katika utekelezaji wa bajeti zetu hizi za serikali. Ni vyema Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu wakavipitia kwa umakini vifungu hivi na tutapovipitisha tuwe na umakini wa kuona umuhimu wake.

Mwisho kabisa nimevutiwa sana na Sehemu ya Kumi na Moja, jinsi gani sheria hii au mswada huu tunaoupitisha hii leo hapa ulivyoweza kuzingatia usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa.

Ni wazi kwamba Serikali zetu za Mitaa zinafanya kazi zao nyingi zinazohusiana na mapato ya fedha zikiwa zinaonekana kama ziko tafauti na mapato ya Serikali Kuu. Lakini ndani ya sheria hii zile zote ni fedha za umma, na usimamizi wake unajulikana ndani ya sheria hii ya usimamizi wa fedha za umma. Hivyo, naona hii ni nafasi pekee na nafasi adhimu kabisa kwa Serikali za Mitaa sasa hivi kuanza kujijua na kuziweka hesabu za serikali katika mtiririko wenye usimamizi bora kabisa.

Huko nyuma ilikuwa inaonekana wazi kwamba fedha za Serikali za Mitaa zinalingana sana na Sehemu ya Kumi na Tatu ya mswada huu iliyokuwa inaonesha ukaguzi na uangalizi wa taarifa za mwaka, kuwa zinakuwa ziko tafauti. Lakini mswada huu tayari unabainisha wazi kuwa serikali imeona jicho lake, imeondoa tafauti juu ya usimamizi wa fedha zile za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Ni pongezi kubwa sana kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuweza kuziunganisha sheria hizi na zikawa sheria moja.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika vifungu mbali mbali nimalizie, nafarajika kuona kwamba sheria hizi sasa zitajali mwenendo na wakati wa matumizi ya fedha. Huko nyuma tulibaini sana serikali kuona kwamba matumizi ya *tender* kwa upande wa Serikali za Mitaa tulikuwa tunatumia kuanza *tender* zinapofikia shilingi milioni tatu, lakini tayari umefika wakati wa kuweka viwango na kuweka fedha ambazo zinakwenda na wakati wa sasa na thamani ya fedha ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hayo machache nashukuru sana kupita kwa mswada huu, na mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Amani tunaunga mkono hoja hii ya mswada huu unaoletwa hapa kwa asilimia mia moja. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na kuniwezesha kusimama hapa kwa mara nyengine tena, lakini mara hii kufanya majumuisho juu ya hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu Mswada wa Sheria mpya ya Usimamizi wa Fedha.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Makamo Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa michango na maoni yao waliyoyatoa na niseme tu, maoni yale tumeyachukua na tutayazingatia katika kurekebisha mswada wa sheria hii.

Nawashukuru Wajumbe wote waliochangia Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa maoni na michango yao yote waliyoitoa.

Mswada huu umechangiwa na Wajumbe 16, 11 wamesema lakini sita wametoa michango yao kwa maandishi. Wajumbe hao ni kama ifuatavyo:-

Waliochangia moja kwa moja:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi, (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo)
2. Mhe. Machano Othman Said
3. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
4. Mhe. Omar Seif Abeid
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi

6. Mhe. Miraji Khamis Mussa
7. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
8. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
9. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
10. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
11. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo

Waliochangia kwa maandishi:

1. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar

Mhe. Naibu Spika, na wawili nitawazungumza baadae, bahati mbaya majina yao yamenitoka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nitoe maelezo juu ya hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, nianze na Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano alizungumza katika kifungu cha 8(2)(d), pale aliulizia iwapo washika fedha wa idara mbali mbali, wizara au taasisi mbali mbali za serikali nao wamo katika orodha ya wale wanaofanya Hazina Kuu ya Serikali.

Jibu ni kwamba, ndio na wao wameorodheshwa wamo katika kile kifungu alichosema cha 8(2)(d), kinawahusisha wahasibu wa idara na taasisi mbali mbali za serikali. Lakini pia alizungumza kwenye kifungu cha 10(1) kuhusiana na majukumu ya Hazina.

Mhe. Naibu Spika, pale alisema suala la rasilimali fedha kuendana na maendeleo ya taifa na alitoa mfano wa suala la matumizi mazuri ya fedha kwenye madawati. Akasema kwamba, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao washirikishwe katika ugawaji huo.

Swali ni zuri na niseme tu kwamba Hazina inafanya kazi zake kwa kuhakikisha maslahi ya taifa yanazingatiwa kikamilifu. Lakini hoja ya kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza washirikishwe katika ugawaji nalo ni jambo zuri, ni jambo jema, lakini hapa itabidi tuweke tahadhari ndogo tu ya kwamba wakati wa ugawaji huo Waheshimiwa Wajumbe sote tuzingatie maslahi ya taifa kwa kuweka vipaumbele kwenye zile wilaya au sehemu ambazo zinaonekana zina mahitaji zaidi kuliko nyengine.

Kwa hiyo, badala ya Waheshimiwa Wajumbe kuja kuvutia majimbo yao au maeneo wanakotoka lazima tuhakikishe wapi kuna mahitaji zaidi na mgao huo uende kwa mujibu wa mahitaji hayo.

Pia Mhe. Machano alizungumzia suala la Wizara ya Fedha kutoa maelekezo kwa taasisi juu ya wapi waweke hesabu za fedha za taasisi zao. Alizungumzia kwamba Tanzania Bara wenzetu wameweka kwenye Benki Kuu. Sasa kwa hili niseme tu kwamba, kwa hapa Zanzibar taasisi zote zinazofungua hesabu za fedha kwa maana ya *account* sharti la mwanzo lazima zipate kibali cha Hazina, bila ya kupata kibali cha Hazina hawawezi kufungua hesabu hizo.

Mhe. Naibu Spika, lakini ndani ya Mswada wa Sheria ambao tunauzungumza kwenye Sehemu ya Tisa, Kifungu cha 56 na 57 kimeelezea utaratibu mzima wa kibenki na yamo masuala ya ufunguzi wa hesabu za fedha katika Sehemu hiyo ya Tisa. Kwa hivyo, tusiwe na wasi wasi suala hilo limezingatiwa vizuri sana na kwa upana zaidi kuliko hata ilivyo katika sheria ya sasa.

Jambo jengine ambalo Mhe. Machano Othman Said amelizungumza ni suala la utaratibu wa taasisi kukopa na kuingia katika madeni. Nalo hili limezungumzwa kwa upana sana katika Sehemu ya Kumi kifungu cha 58 hadi 70 cha Mswada wa Sheria. Na utaratibu huu pia ulikuwepo hapo awali lakini ulikuwepo katika sheria ya mikopo, dhamana na misaada ile sheria ya mwaka 1978. Sasa kimechukuliwa kule kimeletwa kwenye mswada huu wa sheria, lakini hapa kimepanuliwa zaidi kwa kuongezewa nyama katika utaratibu unaohusika.Na tukiangalia kifungu cha 58(3) cha mswada na naomba kunukuu kinasema:

"Taasisi za Umma au Taasisi ya Umma haitoweza kukopa fedha au kutoa dhamana, fidia au kinga katika muamala wowote ambao unalazimisha au unaweza kulazimisha taasisi ya umma au Mfuko Mkuu wa Hazina kulipa fedha baadae isipokuwa mkopo huo, dhamana, fidia, kinga au muamala wowote."

(a) Umeruhusiwa na sheria hii.

(b) Kwa muktadha wa Shirika la Umma umeruhusiwa na sheria yoyote ambayo haipingani na sheria hii.

(c) Umeidhinishwa na Baraza la Mapinduzi.

Kwenye nyaraka ile imeeleza Baraza la Wawakilishi lakini ni Baraza la Mapinduzi kulikuwa na makosa kidogo. Lakini pia kuna suala zima la taasisi zinazopewa ruzuku na mapato, na mapato yao kushuka hili nalo pia lilizungumzwa na Mhe. Machano Othman Said ya kwamba zile taasisi zinazopata ruzuku nyengine huwa zinabweteka na kwa namna hiyo makusanyo ya mapato yao yanashuka. Suala hili ni muhimu na sisi tunaahidi kulifuatilia, na hivyo tutalichukuwa kwa kulifanyia kazi.

Lakini katika kuandaa mipango maandalizi yaanze mapema na kushirikisha wadau wote. Nimwambie tu Mhe. Machano Othman Said ni jambo jema, tumelipokea na tutalifanyia kazi kadri hali itakavyowezekana ili utayarishaji wa mipango uanze mapema, lakini pia ushirikishe wadau mbali mbali. Lakini niseme kwamba Jukwaa la Bajeti na Uchumi moja ya sababu ya kuanzishwa kuhakikishwa kwamba tunatoa nafasi ya kushirikisha maoni ya wadau mbali mbali.

Mhe. Machano Othman Said pia alizungumzia katika kifungu cha 58(2) Mikopo ya nje kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Kama nilivyosema hapa palikuwa na kosa sio Baraza la Wawakilishi lakini ni Baraza la Mapinduzi, na Waheshimiwa Wajumbe wa kamati wameliona na tayari limeshafanyiwa kazi suala hilo.

Sehemu ya 11 Mhe. Machano pia alikuwa na maoni, alisema kwamba ni muhimu kujenga uwezo wa taasisi za serikali za mitaa hasa Mabaraza na Halmashauri. Kwanza tumesema kwamba tutalifuatilia suala hili na kufanya tathmini kwa halmashauri na mabaraza yote kuona uwezo wao ulivyo hivi sasa hilo tutalichukua. Lakini pia kulikuwa na masuala ya kwamba wako wafanyakazi ambao hawajaajiriwa, nao itabidi tubainishe tujue ni halmashauri zipi, mabaraza yepi, wafanyakazi hao hawajaajiriwa na baada ya kufanya zoezi hilo basi tutajua hatua za kuchukuliwa.

Suala la kupunguza riba kwa wafanyakazi wanaopata mikopo kwenye Taasisi za Fedha nalo nikiri kwamba ni suala zuri, ni suala jema, lakini pia itatubidi kwanza tujue hii riba inatoka kwa *base* zipi, na hili tulisema kwamba tunalichukua tutalifanyia kazi, tutakaa sisi na wenzetu wa Benki Kuu kuona kama kuna uwezekano huo wa wafanyakazi wa Taasisi za Serikali kuweza kupata unafuu katika riba wanapopata mikopo kwenye Taasisi za Kifedha.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) nampongeza sana kwanza kwa kusema mambo ambayo ni muhimu na moja alizungumzia suala la kwamba Maafisa wanaosimamia masuala ya fedha lazima wawe na sifa.

Nafikiri kwenye mswada wa sheria hii hilo ni jambo lililosisitizwa kwamba watendaji hawa lazima wawe na sifa na kwenye maeneo tumesema kwamba wawe na utendaji na sifa za viwango vya juu. Lakini suala la taaluma ni suala muhimu na suala ambalo linahitajika kuendelezwa kila mara. Kwa hivyo, nalo hilo tunalichukua tutaangalia jinsi gani watendaji wetu hawa wataweza kupatia taaluma mbali mbali zinazohusiana na masuala ya usimamizi wa fedha.

Pia alizungumza suala la uhaulishaji fedha kutoka kwenye Serikali Kuu kwenda kwenye Serikali za Mitaa. Linalofanyika sasa hivi ni kwamba kwanza tunaangalia yale maeneo ambayo yatafanyiwa ugatuzi kwa maana yatapelekwa kwenye *schedule* yale majukumu yanatahamishiwa kwenye Serikali za Mitaa, na kwa hatua za mwazo serikali imekusudia kugatua maeneo matatu. Kwanza, Elimu ya Msingi, lakini pili Afya na tatu Kilimo. Lakini kilimo kwa upana wake tunazingatia suala zaidi la huduma za ugavi.

Kwa hivyo, kwenye maeneo haya matatu ambayo tutayapeleka kule ndiyo yatakayotusaidia sisi kujua jinsi gani tunaweza tukahaulisha, kwa sababu kama elimu ya msingi basi tutajua mahitaji ya Elimu wa Msingi katika mabaraza na halmashauri nayo sasa tutajua ni kiasi gani kitahitajika kuhaulishwa.

Eneo jengine ni mahitaji ya kiwilaya, wilaya hizi zitakuwa na utafauti wake. Kwa hivyo, zitakuwa na utafauti wa mahitaji kwa mfano idadi ya watu ni tafauti, lakini hata ukija kwenye elimu idadi ya wanafunzi ni tafauti. Kwa hiyo, mahitaji ya uhaulishaji yatakwenda kwa mujibu wa mahitaji ya Wilaya zile au Halmashauri au Mabaraza.
Lakini tatu, tunaangalia pia uwezo wa mapato wa Halmashauri zile na Mabaraza. Kwa maana ile *physical capacity*. Sasa hilo nalo tutaliangalia ili kujua kama wilaya ina uwezo wa kupata mapato yake ule upungufu ni kiasi gani ambao utaweza kuhaulishwa kutoka Mfuko wa Serikali.

Eneo la nne ambalo tutaliangalia ni kiwango cha umasikini, ziko wilaya ambazo hali ya umasikini ni mkubwa zaidi kuliko wilaya nyengine. Kwa hivyo, nayo hiyo itatusaidia katika kufikiria ni kiasi gani cha kuhaulishwa katika wilaya hii. Lakini pia alizungumza suala la Waziri kutangaza mapema kanuni, nimwambie tu na nimuhakikishie kwamba mara tu baada ya kupita sheria hii basi mchakato wa kuanza kutunga kanuni unaanza hapo hapo. Kwa hivyo, hakutokuwa na ucheleweshaji Mhe. Naibu Spika, tutalifanyia kazi kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuhakikisha kanuni hizi zinakuwa tayari kwa haraka kadiri itakavyowezekana. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Jimbo la Konde yeye alizungumzia suala la vigezo vya kudhibiti deni. Sasa hapa nina vigezo vitatu ambavyo tunavitumia katika kudhibiti deni la taifa. La mwanzo ni uwiano wa deni na mapato ya taifa hicho ni kigezo cha mwanzo na inavyotakiwa deni lisizidi asilimia 50 ya pato la taifa. Hicho ndio kikomo cha juu na kwa sasa hivi sisi tuko katika asilimia 17 hadi 18 ya pato la taifa.

Kwa hiyo, serikali yetu bado ina nafasi ya kukopa zaidi. Lakini suala la kukopa pamoja na kwamba tunayo nafasi tunalichukua kwa tahadhari, kwa sababu kukopa ni *liability* kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Kwa hiyo nafasi bado tunayo lakini tunaangalia kukopa pale ambapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Kigezo chengine cha udhibiti wa madeni tunaangalia uwezo wetu wa kukopa, lakini sio wa kukopa tu na wa kurejesha deni, tunao uwezo wa kurejesha deni hilo litarudi kwa miaka mingapi. Kwa hivyo, hicho nacho ni kigezo chengine ambacho tunakitumia katika udhibiti wa madeni.

Tatu, mapato yanatokana na mauzo ya taifa, mauzo ya nchi yetu nje ya nchi nacho hicho pia tunakitumia katika kudhibiti mapato na madeni ambayo taifa letu linaingia.

Suala jengine ambalo alilizungumza Mhe. Omar Seif Abeid ni mkakati wa kudhibiti wakandarasi wanaoshindwa. Hapa niseme kuna njia tafauti kwa wale wakandarasi ambao wanashindwa kutekeleza majukumu yao inapohitaji serikali kurejesha fedha zake kutoka kwa makandarasi hao.

Moja kabisa tunatumia njia ya dhamana za kibenki ambayo makapuni au wakandarasi hawa wanaweka, kwa maana zile *advance* na *performance bond*. Kwa hivyo, wanaposhindwa inabidi sisi turudi benki na kuweza ku- *recover* pesa zetu kutokana na dhamana waliyoweka kutokana na ile fedha wanaolipwa mwanzo, lakini vile vile na *performance* ya utendaji wao.

Lakini la pili, tunazuia mali zao, na pale inapobidi kuzipiga mnada ili kuweza kurejesha pesa hizo. Lakini nji ya tatu kutumia Mahakama. Inabidi tupeleke kesi kudai haki yetu, lakini na nne ambalo ni njia ambayo tunayoipendekeza sasa ni kwamba lazima tusimamie vyema mikataba yetu, na mikataba hii toka hatua ya kuandaliwa suala la uadilifu linarudi kwamba lazima tuwe waadilifu katika hatua za mwanzo za uandaaji wa mikataba, na serikali imetoa agizo kwa taasisi zote kuhakikisha kabla ya kuingia katika mikataba basi mikataba hiyo inafikishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inaangaliwa vizuri ili kuona maslahi ya taifa letu yanalindwa.

Pia, Mhe. Omar Seif Abeid alizungumzia suala la tafsiri ya neno Fungu la Bajeti. Humu imeandikwa tafsiri ni kwamba fungu la bajeti ni taasisi inayotegemea bajeti katika sheria ya matumizi. *Definition* ile aliitilia wasi wasi kidogo, kwamba fungu la bajeti ni kwa nini iwe taasisi. Sasa kwa maana ya mswada wa sheria hii ndio tafsiri ambayo tumeiona inafaa, na hata ukienda kwenye *vision* ya Kiingereza inazungumzia zile *budget institution* na unazungumzia ile fungu kubwa kwa maana ya kwamba kwa mfano kama Wizara ya Fedha ina *votes* tatu, kwa hivyo, kila *vote* ni taasisi. Tume ya Mipango kwa mfano kwenye Wizara ya Fedha ina *vote* yake, kwa hivyo ile ni taasisi, Tume ya Mipango ina *vote* yake, Wizara ya Fedha nayo ni taasisi *by it self* ina *vote* yake nayo Mfuko Mkuu wa Serikali nao ni taasisi kwa sababu ina *vote* yake.

Kwa hiyo, tafsiri inayotafsirika hapa ni tafsiri kwa mujibu wa matumizi ya sheria hii, na ndio maana imewekewa ufafanuzi wa lile neno fungu la bajeti. Kwa hivyo, ukisoma ile tafsiri utapata maana halisi iliyokusudiwa kwa muktadha wa Mswada wa Sheria hii.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza) yeye alizungumzia suala la Mfuko wa dharura *emergency fund* ambayo iko kwenye kifungu cha 54, kifungu kidogo (i) hadi (iv) na yeye hapa alikipongeza kifungu hichi lakini alitaka tuangalie maeneo ambayo fedha hizi za dharura zitatumika na alitaka kwamba basi maeneo hayo tuyaweke ndani ya kanuni. Wazo lake ni zuri na tunalichukua, tutazingatia wakati tutakapotayarisha kanuni, yako maeneo ambayo tunajua kabisa kwamba haya ni maeneo ambayo yakitokea yanaweza kuwa ni hali ya dharura. Kwa hivyo, hayo tunayazingatia kwenye kanuni ingawaje dharura zinaweza zikatokea nje ya maeneo hayo, lakini kifungu tutakiweka vizuri ndani ya Kanuni ili kuhakikisha yale mawazo yake tunayatekeleza.

Suala jengine la Mhe. Miraji Khamis Mussa ni mifumo tofauti baina ya taasisi ameona kwamba katika kutoa taarifa taasisi mbali mbali zinatumia mifumo tofauti pale wanapotoa taarifa za hali ya fedha, na niseme tu kwamba utafauti huo kwanza unatokana na *nature* ya taasisi zenyewe. Lakini ziko taarifa ambazo za msingi ambazo taasisi zinatakiwa kuzitoa katika taarifa zao za kifedha na moja ni kutoa taarifa kuhusiana na mezani ya hesabu kwa maana ya *balance sheet*, lakini vile vile muhtasari wa faida na hasara (*income statement)* na muhtasari wa mwenendo wa kifedha. Hizi ndizo taarifa ambazo zinatakiwa kwa taasisi kuweza kuzitoa taarifa za kifedha. Lakini zinaweza kutafautiana kimaelezo kutokana na *nature* ya ile taasisi yenyewe. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi kwenye hili.

Pia Mhe. Miraji Khamis Mussa alizungumzia kwenye kifungu cha 123 alizungumzia kwamba ukaguzi wa *CAG* unaofanywa *ZRB* unahusisha ile *percent* tu ambayo inatumiwa kwa ajili ya uendeshaji wa chombo kile. Lakini hawafanyi ukaguzi kwa maana ya yale mapato ya jumla yanayokusanywa na *ZRB*. Hapa niseme taarifa zinazokusanywa zinajumuisha pia makusanyo ya mapato ya serikali yanayokusanywa na *ZRB*, na hivi karibuni wameshakamilisha ukaguzi, na naamini kwamba taarifa hiyo itaitishwa hapa mara baada ya kukamilika ambayo itahusisha fedha za *operation*, lakini vile vile makusanyo ya mapato kwa ujumla wake.

Kwa hivyo, nalo hili asiwe na wasi wasi, lakini kuna suala zima la kwamba taarifa hizo zifikishwe ndani ya Baraza hili nimeshawahi kulitolea maelezo ndani ya Baraza hili Mhe. Naibu Spika, na kuelezea tu kwamba Wizara ya Fedha hivi karibuni ni juzi tu nilisema itatoa *secular* kwa mashirika na taasisi zote zinazohusika kutayarisha taarifa zao za kifedha, na waziri husika kuweza kuziwasilisha ndani ya Baraza hili. Hiyo tumeshaizungumza na iko kwa mujibu wa sheria na ni sehemu ya kutekeleza Sheria ya Mitaji ya Umma.

Mhe. Rashid Shamsi, nampongeza naye pia kwa uchambuzi wake wa kina wa mswada huu na maoni aliyoyatoa. Ila niseme tu kwamba mengi ya zile *typographical errors* alizoziona tayari zimeshafanyiwa kazi na kamati, na nadhani kwenye taarifa ya kamati tutaweza kuona marekebisho ambayo yamefanyika.

Lakini alizungumzia na suala la usimamizi na kwamba alisema kwamba usimamizi bado ni hafifu, maadili ni pungufu na nilizitaja njia mbali mbali ambazo zinapoteza fedha za umma. Nimuhakikishie tu kwamba suala kubwa hapa ni usimamizi wa sheria hii, na hilo tumefungia njuga mwaka huu na inayoendelea kuhakikisha kwamba tunalisimamia vizuri. Lakini mbali ya kulisimamia tu na kujenga maadili na taaluma zinatolewa ili wafanyakazi wanaohusika na usimamizi wa fedha lazima tuwe ni wafanyakazi wenye maadili na kukubali kubadilika. Kwa hivyo, hilo jambo tutalifanyia kazi kuhakikisha hizi kasoro nyingi zilizopo zitaondoka na tuweze kuwa na matumizi mazuri ya fedha za umma.

Mhe. Rashid Shamsi, pia alizungumzia kuhusu kifungu kinachomtaka Waziri kuwasilisha taarifa katika Baraza la Wawakilishi juu ya utekelezaji wa bajeti kila robo mwaka.

Kifungu hichi kipo na ukienda kwenye kifungu cha 53(1) suala hili limewekwa wazi kabisa. Lakini pale kuna masahihisho kidogo yalifanyika mwanzoni

ilikuwa pendekezo ni kwamba kila waziri husika, yaani kila waziri wa sekta aweze kuwasilisha. Sasa tumeona hiyo itakuwa ni kazi kubwa na itachukua muda mwingi sana wa Baraza. Kwa hivyo, tumefanya marekebisho waziri anayehusika na masuala ya fedha atatayarisha taarifa ya jumla na taarifa hiyo itawasilishwa katika Baraza kila baada ya robo mwaka.

Kwenye kifungu cha 9 kweli kulikuwa na neno kwa niaba kwa maana ya Hazina Kuu, waziri kwa niaba lile neno limeingia kwa makosa na tumeliondoa tayari na kifungu cha 17(b) uwezo wa kuajiriwa Muhasibu Mkuu, na hichi nacho kifungu kimerekebishwa na sasa uajiri huu unafunganishwa na Sheria ya Utumishi wa Umma nalo hili tumeliona.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alizungumzia kuhusiana na suala la kazi na uwezo wa waziri, Katibu Mkuu na Muhasibu Mkuu na kutaka kazi zao zitenganishwe.

Naomba nielekeze kwamba mswada wa sheria hii umezitenganisha wazi wazi kabisa kazi, uwezo na majukumu ya waziri, Katibu Mkuu na Muhasibu Mkuu hizo ziko mbali mbali. Lakini mlipaji Mkuu wa Serikali wakati anapoteua alitoa wazo hilo Afisa Muhasibu ambaye siye Mkuu wa Taasisi basi uwekwe muongozo wa kumuongoza Afisa mlipaji katika kufanya kazi hiyo.

Kazi hii inafanyika au utaratibu huu unafanyika pale inapohitajika kwa kuzingatia utaratibu maalumu. Lakini tunaamini kabisa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mara yoyote au kwa wakati wowote atakuwa ni mtu makini, na kwa namna hiyo haitoweza kuchagua Tarishi kumuweka akawa Afisa Mhasibu. Kwa sasa hivi kesi hii imetokea kwenye taasisi tatu. Moja ni Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kwa sababu ya *nature* za kazi za Mhe. Mwanasheria Mkuu zinaingia katika kisiasa. Imeamuliwa kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu ndiye awe Afisa Mhasibu. Kwa hivyo hapo imetokea hivyo na imefanyika kwa kuzingatia hilo. (*Makofi*)

Pia, kwenye Wizara ya Fedha Katibu Mkuu yeye ndiye Mlipaji Mkuu, kwa hivyo hakupaswa na yeye kuwa Afisa Mhasibu kwa wizara ile. Kwa hivyo kazi hiyo sasa imetolewa kwa Naibu Katibu Mkuu. Hivyo Naibu Katibu Mkuu ndani ya Wizara ya Fedha ndiyo Afisa Mhasibu.

Pia Afisi ya Rais Baraza la Mapinduzi nafasi ile ambayo badala ya kuwa Katibu Mkuu Kiongozi ndiyo Afisa Mhasibu na yeye kutokana na majukumu yake, kazi hiyo imetolewa kwa Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo sasa hivi tuna maeneo hayo matatu, lakini kadri itakavyohitajika basi

suala hili litafanywa kwa uangalifu mzuri zaidi, ingawaje angalizo lako tumelisikia. (*Makofi*)

Suala la Msajili wa Hazina. Ndani ya Mswada wa Sheria hii Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri imetajwa, kipo kifungu kinachoonesha kwamba kutakuwa na Msajili wa Hazina na amepewa jukumu, lakini uteuzi wa Msajili wa Hazina tayari ametajwa kwenye ile Sheria ya Mitaji ya *Umma (Public Investment Act).* Kwa hivyo, yupo kule na Mswada wa Sheria hii umefanya *reference* kwenye kifungu kile.

Pia, ulizungumzia suala la kuandaa Kanuni za Maadili *(Professional Codes of Conduct)* kwa Wahasibu, ni wazo zuri na nikuhakikishie tu Mhe. Naibu Spika, kwamba wazo hili tunalichukua na tutalifanyia kazi.

Sheria ya Mapato ifanyiwe mapitio, nayo pia ilizungumzwa na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Sheria za Mapato zipo nyingi na kila inapohitajika tunafanya mapitio na kufanya marekebisho. Kama unakumbuka hivi karibuni tu wakati wa Kikao cha Bajeti tulileta hapa Mswada wa Sheria ya Fedha *(Financial Bill)* ambapo kulikuwa na Sheria mbali mbali zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato zilifanyiwa marekebisho haya.

Kwa hivyo, Sheria zipo nyingi na kila inapohitajika na kila mwaka kupitia Sheria ya Fedha marekebisho hayo yanafanyika.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Said Soud Said, Mhe. Juma Khatib na Mhe. Moudline Castico, Mhe. Rashid Ali Juma, Mhe. Riziki Juma Pembe, Mhe. Shehe Hamad Mattar, wote hawa wametoa maelezo yaliyoongezea nguvu hoja ambayo nimewasilisha hapa. Kwa hivyo, ninawashukuru sana na ninaamini maelezo niliyoyatoa yame-*cover* karibu maeneo yote ya Waheshimiwa Wajumbe waliyotaka ufafanuzi. Ninawashukuru sana na ninawashukuru nyote kwa michango yenu. (*Makofi*)

Na ninaamini Mhe. Naibu Spika, kwamba Wajumbe watapitisha Mswada wa Sheria hii bila ya matatizo. (*Makofi*).

Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa toa hoja. Mhe. Waziri umetoa hoja?

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja, sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tutapitisha Mswada huu kwa mafungu kwa mujibu wa Kanuni ya 87 (3).

Sehemu ya Kwanza	Masharti ya Awali pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Pili	Kazi na Uwezo wa Baraza la Mapinduzi pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Tatu	Hazina ya Serikali pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Nne	Mfuko Mkuu na Mifuko Maalum pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Tano	Dhamana za Maafisa Mhasibu pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Sita	Uandaaji wa Mpango, Bajeti na Uidhinishaji wa Bajeti pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Saba	Utekelezaji wa Bajeti pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Nane	Uanzishaji wa Mfuko wa Dharura pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Tisa	Usimamizi wa Fedha na Utaratibu wa Kibenki pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi	Kukopa, kukopesha na Usimamizi wa Madeni pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Moja	Usimamizi wa Fedha katika Serikali za Mitaa pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Kumi na Mbili	Masharti kwa Mashirika ya Umma pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Tatu	Taarifa ya Mwaka, Ukaguzi na Uangalizi pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Nne	Kufuata Masharti na Adhabu pamoja na marekebisho yake
Sehemu ya Kumi na Tano	Masharti ya Jumla

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nitawahoji tena wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wale wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa utulivu wenu na kwa michango yenu kwa makofi yenu mengi sana. Basi tumuombee Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kila heri katika utekelezaji wa Sheria hii tuliyoipitisha hapa Barazani.

Waheshimiwa Wajumbe tumemaliza shughuli zetu za leo lakini kabla ya kumaliza nina matangazo mawili.

Tangazo la kwanza linatoka kwa Mhe. Spika, ni tangazo linalohusiana na taarifa za utekelezaji wa Wajumbe katika majimbo yao.

Waheshimiwa Wajumbe tunapewa taarifa kwamba ule mpango wa kutoa taarifa za utekelezaji wa Wajumbe katika majimbo kwa kutumia gazeti la Zanzibar Leo hivi sasa upo tayari. Kwa taarifa hii Mjumbe yeyote ambaye yupo tayari awasiliane na Mhariri Mtendaji kwa anuani na namba za simu zilizomo katika gazeti hilo au afike mwenyewe katika Afisi ya Zanzibar Leo iliopo Rahaleo na kuonana na wahusika.

Makala ya taarifa hizi zitaanza kutolewa mwezi wa Januari mwakani. Waheshimiwa tunaombwa sana kuitumia ipasavyo fursa hii ikiwa ni njia mojawapo ya kuhimiza uwazi na uwajibikaji. Anakushukuruni sana Mhe. Spika.

Tangazo jengine ni kuhusu uchaguzi wa *CWP*. Waheshimiwa Wajumbe kutokana na dharura ambayo ilipatikana leo akinamama tulishindwa kufanya uchaguzi wa *CWP*, hivyo Katibu anatangaza kwamba uchaguzi wa *CWP* utafanyika kesho baada ya kikao chetu cha mchana.

Baada ya matangazo hayo mawili, sasa ninatangaza rasmi kwamba Baraza letu tumeliahirisha hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.00 jioni Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 01/12/2016 saa 3.00 asubuhi)